

Elimu-Jumuishi Kwa Vitendo

**Taarifa ya Warsha Kuhusu Elimu-Jumuishi Iliyofanyika
Zanzibar, 7-10 Februari 2006**

“Kujifunza hakuna mwisho.”

“Kazi ya vikundi imenipa fursa ya kujieleza bila kuhofia kuwa ningekosea.”

“Nimeona ubora wa uhusiano wa kirafiki miongoni mwa washiriki wenzangu. Ni kama sote tunatoka nchi moja na siyo kutoka sehemu mbalimbali za dunia.”

“Washiriki wote walionekana kama familia moja (kukubaliana na kuheshimiana)”

“Kadri siku silivyoendelea, washiriki walianza kujitokeza na sasa wanaweza kujadili masuala mbalimbali kwa uhuru na uwazi.”

“Ninapenda kazi za matendo ambazo huwafanya washiriki wakumbuke yale yaliyotendwa katika warsha, na pia huwasaidia kurudi katika warsha wakiwa na nguvu mpya.”

“Ni lazima tukumbuke kila siku kwamba elimu ni haki ya wote, na hatuna budi kuipata – tuisubiri mpaka tupewe na watu wengine.”

Maoni ya washiriki kuhusu warsha

Ripoti hii imechapishwa na:

The Atlas Alliance
Schweigaardsgt 12
SLP 9218 Grønland
0134 Oslo, Norway
Simu: +47 22 17 46 47
Faksi: +47 23 16 35 95
Barua pepe: atlas@atlas-alliansen.no
Tovuti: www.atlas-alliansen.no

Toleo la kwanza: 12 Machi 2007

Mwandishi wa ripoti: Ingrid Lewis

Upatikanaji: Ripoti hii inapatikana kwenye tovuti ya shirika la ‘Atlas Alliance’ (www.atlas-alliansen.no) na tovuti ya shirika la ‘Enabling Education Network’ (www.eenet.org.uk)

Inapatikana pia kwenye machapisho ya breili (Braille) na kwa Kiswahili kutoka shirika la ‘Atlas Alliance’.

Yaliyomo

Shukurani	2
Vifupisho	3
1. Utangulizi	4
1.1. Warsha ililenga yafuatayo	4
1.2. Ni watu gani walioshiriki?	4
1.3. Ni njia zipi tulizotumia?.....	5
2. Elimu-jumuishi ni nini?	6
2.1. Kufasiri dhana ya ‘elimu-jumuishi’	6
2.2. ‘Elimu-jumuishi’ inaonekanaje?	11
2.3. ‘Elimu-jumuishi’ ni mchakato endelevu	13
2.4. Elimu-jumuishi humaanisha <i>kuwepo, kushiriki na kunufaika</i>	14
3. Vikwazo na ufumbuzi wake	18
3.1. Kubainisha vikwazo vya ujumuishi’ na wanaoathiriwa navyo.....	18
3.2. Ufumbuzi wa vikwazo/matatizo	20
3.3. Wanasemina walitaja vikwazo na ufumbuzi gani?	20
4. Hatua zinazofuata	41
4.1. Kubainisha vikwazo maalum na ufumbuzi wake	41
4.2. Kutumia utafiti-kwa-vitendo	42
5. Ufupisho wa masomo na mapendekezo	45
6. Matokeo ya warsha	50
Maelezo ya mawasiliano ya washiriki	50
Mapendekezo ya marejeo	56
Kuhusu wafadhili na waandaaji wa warsha	57

Shukurani

Timu ya waandaji wa warsha inapenda kutoa shukurani kwa washiriki wote waliochangia uzoefu, mawazo, matumaini, changamoto na hadithi za kuisimua, na ambao hawakuchoka kuuliza maswali kwa kipindi chote cha siku nne za warsha, Zanzibar.

Shukurani mahsusi zimwendee Ingrid Lewis wa “*Enabling Education Network (EENET)*” ambaye alishiriki kikamilifu wakati wazo la kuendesha warsha hii lilipotolewa kwa mara ya kwanza. Aliandaa na kuwezesha kufanyika warsha hii, na kila mara alirudia agenda ya kuangaliwa kwa mahitaji ya washiriki. Kisha aliandika na kuhariri taarifa.

Shukurani zetu za dhati pia ziwaendee waendeshaji wenzetu ; Edwina Mulenga Mumba na Patrick Kangwa, walimu kutoka Mpika, Zambia. Michango yenu ilitia chachu ya kutosha.

Tunapenda kutoa shukurani zetu kwa wizara ya Elimu Zanzibar - hususan ofisi ya Elimu Maalum (kwa sasa, kitengo cha elimu-jumuishi) kwa kuikarimu warsha hii, na vilevile shukurani zetu kwa Chama cha Watu wenye ulemavu Zanzibar (ZAPDD) ambacho kilihakikisha kila kitu katika warsha kilienda vizuri kama kilivyopangawa. Tunapenda hasa hasa kumpa shukurani zetu za dhati waziri wa Elimu Mh. Haroun Ali Suleiman kwa kufungua semina na kuitangaza rasmi sera ya ‘elimu-jumuishi’ katika Zanzibar.

Na hatimae, shukurani maalum kabisa ziende kwa “*Operation Day’s Work*” kwa kutoa msaada wa kifedha kwa ajili ya uendeshaji wa warsha na uchapishaji wa taarifa hii.

Timu ya waandaji:

Silje Handeland, Norwegian Association for Persons with Developmental Disabilities (NFU)

Bergdis Joelsdottir, Norwegian Association of Disabled (NAD)

Berthe Stenberg, Line Thorgersen and Trond Berget, the Atlas Alliance Secretariat.

Vifupisho

CBR	community-based rehabilitation (uwezesaji ki-jumuiya)
DPO	disabled persons organisation (chama cha wasiojiweza)
EENET	Enabling Education Network (Mtandao wa Uwezesaji Katika Elimu)
MIEP	Malawi Inclusive Education Project (Mradi wa Elimu-jumuishi Malawi)
MOET	Ministry of Education and Training (Lesotho) (Wizara ya Elimu na Mafunzo (Lesotho))
NAD	Norwegian Association of Disabled (Chama cha Wasiojiweza Norway)
NGO	non-governmental organisation (shirika lisilo la serikali)
NFU	Norwegian Association for Persons with Developmental Disabilities (Chama cha Watu Wenye Ulemavu Norway)
TAMH	Tanzania Association for Mentally Handicapped (Chama cha Watu Wenye Mtindio wa Akili Tanzania)
ZAPDD	Zanzibar Association for People with Developmental Disabilities (Chama cha Watu Wenye Ulemavu Zanzibar)

1. Utangulizi

1.1. Warsha ililenga yafuatayo

- Kwawezesha wanasemina kujifunza na kubadilishana uzoefu na mawazo kuhusu kupanga, kutekeleza na kudurusu/kutathmini kazi za elimu-jumuishi katika muktadha wa nchi inayoendelea.
- Kuonesha njia shirikishi za kujifunza (katika warsha) ambazo pia zinaweza kutumika katika uongozi wa projekti na mazoezi darasani ili kiwashirikisha na kuwajumuisha zaidi washiriki.
- Kuwasaidia wanasemina kufikiri na kuendeleza mipango yao kwa maendeleo zaidi kuhusu elimu-jumuishi.

1.2. Ni watu gani walioshiriki?

Waandaaji na wafadhili

Warsha iliandaliwa na watumishi kutoka makao makuu ya ‘Atlas Alliance’, NAD na NFU yote ya Norway, na kusaidiana na wafanyakazi wenyeji wa nchini kutoka ZAPDD ambalo ni shirika-mwenzaji la NFU la Norway. Fedha za uendeshaji wa warsha zilitolewa na ‘Operation Day’s Work’. Wizara ya Elimu na Mafunzo walikuwa maafisa wenyeji wa warsha wakisaidiana na ZAPDD.

Washiriki

Jumla ya washiriki 42 walihudhuria warsha (ikiwa ni pamoja na waendeshaji na waandaaji). Wengi wao walitokea NFU na NAD ambayo ni mashirika-wenzaji. Washiriki wengine walikuwa wa kutoka katika projekti za elimu-jumuishi walioalikwa kutoka mashariki na kusini mwa Afrika. Hawafanyi kazi moja kwa moja katika NAD na NFU, bali uzoefu wao ulikuwa muhimu katika warsha. Kwa pamoja, 30 walitoka Afrika, 9 walitoka Norway, 1 kutoka Nepal, 1 kutoka Palestina na 1 kutoka Uingereza. Orodha kamili ya washiriki ipo ukurasa wa 50–55.

Waendeshaji

Mwendesha semina mkuu alikuwa Ingrid Lewis ambaye ni mratibu wa EENET. Patrick Kangwa na Edwina Mulenga Mumba walikuwa waendeshaji wasaidizi. Wote wawili walikuwa walimu wa shule za msingi kutoka ‘shule za elimu-jumuishi’ za Mpika, kaskazini mwa Zambia. Wamekuwa wakifanya kazi na EENET kwa miaka mingi kuhusu uendelezaji wa njia za Utafiti-kwa-Vitendo (*action research*) kwa ajili ya elimu-jumuishi.



Washiriki na waandaaji wa warsha

1.3. Ni njia zipi tulizotumia?

Warsha iliandaliwa kiasi kwamba katika mchakato wa kutoa habari kuhusu elimu-jumuishi ingesaida pia kuonesha njia za kujifunza na kufundishia ambazo husadifu darasa-mchanganyiko (jumuishi). Matendo mengi yalikuza kujifunza kwa vitendo na kujenga moyo wa kujiamini katika kujifunza, badala ya kumtegemea mwalimu au mkufunzi tu katika somo. 'Elimu-jumuishi' siyo dhana rahisi kiasi kwamba inaweza kutumiwa kwa namna moja sehemu zote. Hivyo, haiwezikani na wala haipaswi kwa mkufunzi kuwakaririsha wanasemina maana ya 'elimu-jumuishi' na namna inavyo tekelezwa.

Warsha ilitumia kazi za vikundi/jozi, majadiliano ya wazi na uwasilishaji wa kazi. Njia zote hizi zilitumika ili kuhakikisha kuwa washiriki wote wanashirikishwa kwa staili mbalimbali. Hii inaaksi jinsi darasa la elimu-jumuishi linavyopaswa kuendeshwa.

Zaidi ya hayo, warsha ilisisitiza kuwa mwalimu huhitaji kujifanya mahiri wa 'elimu-jumuishi' kwa kufanya matendo kwa lengo la kufanya elimu iwe jumuishi zaidi. Kumbuka kila mmoja ana mawazo na uzoefu aliopata katika kazi na maisha yake ya kila siku ambapo mambo aliyonayo yanaweza kuwa muhimu sana katika mfumo wa 'elimu-jumuishi' na jamii.

Taarifa ndogo (sambamba na hii) inayoonesha bayana matendo yaliyotumiwa ama kutekelezwa wakati wa semina, inapatikana pia. Katika taarifa hiyo, kuna maelezo ya kina kuhusu njia zilizotumika kuwashirikisha wanasemina wote kwa pamoja (nusu-siku ya mwanzoni mwa warsha ilitumika kwa 'stadi ya mawasiliano'). Na vilevile habari kuhusu mbinu-shirikishi zilizotumika kupata maelezo yaliyomo katika taarifa hii, imo katika ripoti hiyo ndogo.

2. Elimu-jumuishi ni nini?

2.1. Kufasiri dhana ya 'elimu-jumuishi'

Washiriki walitaja orotha ifuatayo katika kutafsiri dhana ya 'elimu-jumuishi':

- elimu kamili kwa wote
- usawa
- kuondoa vikwazo katika kujifunza
- ni mchakato endelevu
- kuwapa walimu stadi za elimu maalum
- mfumo unaojumuisha wanafunzi wenye mahitaji mbalimbali
- kuanzisha mfumo wa shule kwa watoto wote
- kuelewa uwezo anuwai wa wanafunzi.
- kuheshimu tofauti zetu
- elimu kwa wote
- kukubaliana
- kuthaminiana
- kusaidiana
- uhuru wa kuwasiliana na kucheza.

Washiriki pia walioneshwa tafsiri ya 'elimu-jumuishi' ya *EENET* iliyotolewa na washiriki mbalimbali kutoka nchi mbalimbali waliohudhuria warsha kama hii Agra, nchini India mwaka 1998, kama ifuatavyo:

- watoto wote wanaweza kujifunza
- 'elimu-jumuishi' ni mchakato shirikishi unaowashirikisha wanafunzi wote katika kujifunza
- tofauti za watoto- mf, umri, jinsia, kabila, lugha, ulemavu, UKIMWI na Kifua Kikuu - lazima zitambuliwe na kuheshimiwa
- miundo, mifumo na njia za utoaji elimu lazima viandaliwe na kuendelezwa ili kukidhi mahitaji ya watoto wote
- mambo yote hayo lazima yafanywe kuwa sehemu ya mkakati kabambe wa kuendeleza 'elimu-jumuishi'
- wingi wa wanafunzi darasani au uhaba wa vifaa uya elimu si lazima viwe vikwazo katika 'elimu-jumuishi'.


Washiriki walihisi kuwa dhana zifuatazo hazikuigingizwa katika fasiri hizo:

- kutambua na kuthamini namna watoto wanavyojifunza na kuwasiliana baina yao
- umuhimu wa kuishirikisha jamii.

Wakati wa majadiliano yote hayo, ilisisitizwa kwamba hakuna tafsiri moja ya 'elimu-jumuishi' ambayo inaweza kusadifu kila mahali. Elimu-jumuishi ni dhana inayoshirikisha kufuatana na mazingira. Warsha haikutaka kuwakaririsha wanasemina fasiri maalum. Na wala haikutaka wanasemina wakubaliane na maana moja maalum ya dhana hiyo. Badala yake iliwahamasisha kufikiri katika upana wa dhana ya 'ujumuishi' na mambo yanayoweza kuchagiza 'elimu-jumuishi' kutegemeana na miktadha mbalimbali.

Tatizo liko wapi?


Vielelezo vifuatavyo vilioneshwa. Kielelezo cha kwanza kinaonesha jinsi mfumo wa elimu ya jadi ulivyokuwa unawatazama watoto wenye tofauti/ulemavu mbalimbali. Mtoto anaonekana kama ndiye tatizo, kitu ambacho kinatufanya tutafute ufumbuzi wa kumbadili mtoto, kujaribu kumponya, au kumfanya aingie na kukubalika katika mfumo wa elimu uliopo.



Kielelezo cha pili kinaonesha njia mbadala. Hapa mtoto hachukuliwi kama tatizo. Mfumo wa elimu ndio tatizo kwa kuwa hauna namna ya kuruhusu watoto wa aina zote za tofauti kuingia.



Kielelezo cha tatu pia kilioneshwa. Tukiona mfumo wa elimu kama ndio tatizo, basi tunapaswa kubuni ufumbuzi wa tatizo hilo. Hatumrekebishi mtoto kuingia katika mfumo; badala yake tunabadili mfumo wa elimu ili uweze kuhudumia na kuwa kwa 'manufaa ya watoto wote'.



Majadiliano Yaliyotokana na Vielelezo

Vielelezo hivyo vilichochea majadiliano miongoni mwa washiriki kuhusu maana ya 'elimu-jumuishi' na changamoto zake. Ufupisho wake ni kama ifuatavyo:

Motisho na maslahi kwa walimu

Vielelezo vinaashiria kuwa 'elimu-jumuishi' ni, au inapaswa kuwa, changamano yenye kuhitaji mabadiliko mengi. Walimu mara nyingi husema hawataki kujitwisha mzigo zaidi wa 'ujumuishi' (la sivyote, wangepaswa kulipwa zaidi kwa kufanya hivyo). Tunawamotishaje walimu hawa ili wafanye kazi wanayofikiri inahitajika? Hili ni tatizo la dunia nzima, na hasa katika nchi ambazo mifumo yake ya elimu inalenga zaidi kufaulu mitihani na ushindani wa mashule (Uingereza na Kenya zilitajwa kama mfano).

Mfano wa mwalimu wa Bahamas ulitajwa. Mfano huu ulionesha kwamba kwa kutumia njia za kufundishia na kujifunza ili kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum, tunakuwa tunawaendeleza kielimu watoto wote. Hii inaweza kuhamasisha walimu. Mwalimu Bahama anatumia tathmini yake kwa wanafunzi wake darasani. Wanafunzi hujipima kwa vigezo vyao wenyewe na namna yao ya kutathmini na kusahihisha kazi zao. Mbinu hii ilitumika ili kuwaingiza hata wanafunzi waliokuwa katika hatari ya kutengwa au kuachwa (mf. wanafunzi wasiojiweza ambao hawawezi kuikabili mitihani migumu na njia mbalimbali za kueleza mambo wanayojifunza). Hata hivyo inasaidia wanafunzi wote. Mwalimu aliona kuwa baada ya juhudi zake za awali za kujenga na kuendeleza njia hii, sasa ni mwalimu mzuri na wanafunzi wake wote wanafaulu vizuri katika mitihani rasmi.

Mitihani

Mwanasemina mmoja alihisi kuwa kielelezo cha *Mazingira ya shule kwa ajili ya watoto wote* kingepaswa kuingiza kipengele cha *Ushirikishwaji wa bodi ya mitihani*. Hii ingewadhihirishia kuwa wanawafahamu wanafunzi wao na kuwafikiria katika mitihani, kwa mfano kuwasaidia wale wanaosuasua kwa kuwaongeza muda zaidi; au kuwapa mtihani kwa mdomo (kuzungumza) wale wasioweza kuandika; au kutumia njia mbalimbali za kutathmini maendeleo yao.

Mwanasemina mmoja alisimulia kuhusu mtu mmoja aliyekuwa na mtindio wa akili ambaye alifeli mtihani mara tatu kwa kushindwa kuandika. Aliporuhusiwa kuujibu kwa mdomo alijibu maswali yote kwa usahihi. Baadaye alijifunza kuchapa kwa mashine.

Tatizo la waajiri kuthamini mitihani ya mdomo, na kwamba shule-jumuishi zinaweza kuwaandaa wenye ulemavu kwa ushindani katika soko la ajira, ni mambo yaliyojadiliwa pia. Ilielezwa kwamba 'shule-jumuishi' na jamii-jumuishi (mf. sehemu mbalimbali za kazi) huenda sambamba. Kwa hiyo kadri mfumo wa elimu unavyobadilika ndivyo pia jamii inayoizunguka shule inavyopaswa kubadilika (na kinyume chake ni sawa). Na zaidi ya hayo, elimu ni kujifunza stadi za maisha na siyo sifa tu za kitaaluma tunazoweza kupata – na hii lazima isisitizwe katika elimu (mashuleni) na jamii kwa jumla.

Watoto wenye kipaji maalum

Athari ya 'elimu-jumuishi' kwa watoto wenye uwezo wa juu sana (kipaji maalum) – katika jamii ambayo wazazi wanashindana kuwapa watoto wao elimu bora zaidi ilijadiliwa wakati wa kujadili vielelezo hivi. Je, mchakato huu wa kuelekea 'elimu-jumuishi' unaweza kuwafaa pia wanafunzi wenye vipaji maalum (kiakili) ambao husahaulika? Wanasemina walijadili kuwa, walimu daima hupaswa kuandaa na kufukiria mahitaji ya wanafunzi wote darasani; wote wasiojiweza na wale wenye vipaji vya juu. Tunatakiwa kuwashawishi walimu kuwa 'elimu-jumuishi' haimaanishi mzigo mpya, bali badala yake inawapa njia mpya za kufundisha wanafunzi wa madarasa ya juu au wale wenye uwezo zaidi kusaida kufundisha wale wasiojiweza wanaojitahidi kujifunza, siyo tu inawasaidia 'wanafunzi wanaojifunza taratibu', bali pia inawanufaisha hawa wenye uwezo wa juu kwani kwa kuwafundisha wenzao hufanya marudio ya masomo yao pia.

Uzoefu binafsi kuhusu kubadili njia yangu ya kufundisha

Nilikuwa na wanafunzi 45-50 katika darasa langu. Sikuwa nafuatilia wale wenye uwezo mdogo darasani. Sikuwajali kabisa. Nilikuwa nikiandaa somo kwa wote bila kujali tofauti zao na kuwaona sawa tu. Sikufikiria namna tofauti ya kufundisha. Lakini idadi yao darasani ilianza kupungua. Baada ya kupata mafunzo ya 'Elimu (ya mahitaji) maalum' na kujifunza juu ya 'elimu-jumuishi', niligundua kuwa nilitakiwa kuandaa somo kwa kuzingatia mahitaji yao maalum. Ukiwaonesha watoto upendo, kuwajali na kujihusisha nao, watoto watakuja shule kila siku. Lakini usipowaonesha vyote hivyo, hawataendelea na shule. Unapowaleta karibu yao, watapenda shule. Usipowashirikisha nao hawatashiriki darasani. Usiwapuuze watoto - waulize nini wangependa kujifunza kutoka kwako – wana uzoefu wao katika mambo, na hivyo anzia hapo kuwafundisha.

Mwanafunzi mmoja niliyekuwa nikimchukulia kama mwenye uwezo mdogo wa kujifunza, aliniuliza “naomba unifundishe namba hii '27'. Je ni namba moja au mbili tofauti?” Ilikuwa ni kazi kwangu kutafuta jinsi ya kufanya ajifunze namba hii kwa urahisi. Hakuna haja ya kuchagua wakati wa ufundishaji wetu. Na wala siyo suala la wenye ulemavu, wenye uwezo mdogo wa kujifunza, au wenye kutupa changamoto kwa vipaji vyao, ndio wanaohitaji ufuatiliaji maalum, la hasha. Kila mwanafunzi anahitaji kujifunza na kupata kitu kipya atokapo shuleni.

Edwina Mulenga Mumba (Zambia)

Wanafunzi wenye mimba

Kama sehemu ya zoezi la chemsha-bongo¹, wanasemina walishiriki katika mdahalo uliohusu wasichana wa shule wenye mimba kuachishwa masomo au la; au kama 'elimu-jumuishi' maana yake ni pamoja na kuwaruhusu kuendelea na shule. Karibu 25% ya washiriki waliona ni heri waachishwe shule, na 75% walisema bora waachwe waendeleo na masomo na pia waingizwe katika mfumo wa elimu-jumuishi. Kulikuwa na mdahalo kuhusu mwanafunzi mwenye mimba kama anaweza kurudi shule kuendelea na masomo akiachishwa. Baadhi ya shule au nchi huwafukuza moja kwa moja wasichana wenye uja-uzito. Wanasemina pia walijadili uwezekano wa athari ya kisaikolojia itokanayo na dhihaka wanafunzi waja-wazito waachwapo waendeleo na shule. Washiriki wengi waliona kuwa ni wajibu wa shule kuwalinda dhidi ya dhihaka na kejeli, badala ya kuwaachisha masomo. Masuala ya kiafya pia yalitajwa kama moja ya sababu za kuwaachisha shule. Wapinzani wa upande huu walidai kwamba, kwa kuwa shule inategemewa kuwa na huduma ya kutosha kwa wanafuuzi wasiojiweza au wagonjwa, kwa nini afya ya wanafunzi waja-wazito isihudumiwe vivyo hivyo. Suala la elimu kuwa haki ya watoto wote nalo liliibushwa. Mshiriki mmoja alihitimisha kwa kusisitiza kwamba tunapozungumzia 'ujumuisho' katika elimu tunazungumzia kujumuisha watoto wote, na kwamba kumjumuisha mwanafunzi mjamzito hakuna tofauti na kumjumuisha mwanafunzi mlemavu au mtoto mkimbizi.

¹ Zoezi la chemshabongo liliitwa “kubali-sikubali” kwa maelezo zaidi, tazama ripoti ndogo kuhusu njia za warsha.

2.2. 'Elimu-jumuishi' inaonekanaje?

Hakuna kanuni maalum ya kuifanya 'elimu-jumuishi' ionekane. Kuna mabadiliko makubwa na madogo tunayoweza kufanya ili kuifanya shule ionekane ni 'jumuishi'zaidi. Mabadiliko mahsusi tunayohitaji kila mmoja wetu yanategemeana na hali iliyopo shuleni au mfumo wa elimu na watu waliomo katika mfumo au shule husika. Vilevile hakuna alama moja (tu) inayoweza kuashiria namna 'shule-jumuishi' au mfumo wake wa elimu ulivyo. Kila shule/mfumo unaweza kuwa na lengo kuu la haki sawa ya elimu kwa wanafunzi wote. Lakini jinsi ya kutimiza lengo hilo inatofautiana shule na shule, na hata nchi na nchi.

Wakiwa katika vikundi vidogo vidogo, wanasemina walizichunguza picha za shule kutoka Zambia na Indonesia kuwasaidia kuelewa (wao wenyewe) mambo yanayoifanya shule iwe 'jumuishi' au la. Picha hizo, nyingi zilipigwa na wanafunzi kama sehemu ya mradi kuonesha 'ujumuishi' katika shule zao². Zoezi hili pia liliwakumbusha wanasemina kuwa tunayoyaona kwa nje hayatupi mambo yote tunayohitaji katika 'mfumo-jumuishi'. Tunapaswa kuchunguza kila hali kwa makini kabla hatujachambua na kupendekeza mabadiliko.

Mawazo ya wanasemina kwa ufupi kuhusu 'elimu-jumuishi' inavyopaswa kuonekana:

Picha	Ni jumuishi kwa sababu:	Siyo jumuishi kwa sababu:	Mawazo ya mpiga picha
	Ardhi ni tambarare, panafikika.	Sioni watoto walemavu; Baadhi ya watoto wame-tengwa.	Mwanafunzi wa kike: "Napenda kutazama mpira wa miguu, siyo kucheza; napenda kiwanja, ni sehemu ya michezo, inanivutia kujashunie".
	Mlemavu ni mwalimu, shule inafikika, hakuna wanafunzi walemavu pia safi.	Anayeonekana mlemavu ni mzazi, na mwalimu anaongea naye kwa ukali; hii inaonesha hakuna ukaribu kati ya walimu na wazazi	Mwanafunzi wa kiume; "inaonesha walimu wangu wawili, na walimu wakiwasiliana ni vizuri".

² Kwa maelezo zaidi kuhusu namna zoezi hili lilivyofanyika, tazama ripoti ndogo ya njia za warsha

Picha	Ni jumuishi kwa sababu:	Siyo jumuishi kwa sababu:	Mawazo ya mpiga picha
	<p>Ni darasa-jumuishi lenye uhuru na demokrasia; mwalimu anatembea nyuma na mbele kuwasaidia wanafunzi, hasimami mbele tu, wanafunzi wamefurahi</p>	<p>Mwalimu kawapa mgongo wanafunzi walio nyuma yake wanaweza kucheza au kuongea ovyo.</p>	<p>Mvuulana: “Picha hii inaonesha nijisikie vizuri shuleni, mwalimu wangu daima ni mwema na anasaidia sana”.</p>
	<p>Kuna mwanafunzi zeruzeru darasani. Wanafunzi wote wanafurahia jambo mbele ya darasa. Ni darasa zuri.</p>	<p>Inawezekana zeruzeru ni mlemavu wa macho na kawekwa nyuma ya darasa; hakuvaa sare ya shule; ni rahisi kudhihakiwa kwa kutovaa sare.</p>	<p>Mtafiti mtu mzima: “Darasa linajifunza kwa kazi-vikundi. Hakuna viti vya kutosha, lakini wanapishana kuketi”.</p>
	<p>Hakuna ngazi-ngazi vyooni; na hivyo vinafikika na watoto wote kwa urahisi.</p>	<p>Vyoo havifikiki kwa urahisi kwa sababu korido zake ni ndogo mno na hakuna milango (hakuna siri) hakuna njia pia.</p>	<p>Mwanafunzi: “shule ni jumuishi sasa. Zamani hatukuwa na vyoo wala sehemu za kujificha (hakukuwa na michongoma).</p>
	<p>Vibao/mabango haya yanaonesha jinsi mwalimu anavyo hamasisha ushirikishaji wa wanafunzi.</p>		<p>Mtafiti Mtu mzima: “Wanafunzi walieleza kwamba walifurahishwa na jinsi mwalimu wao anavyowapa uhuru wa kuuliza na kutaka wasome nini kesho yake, n.k.”</p>
	<p>Kila mmoja anaonekana akishiriki na kufurahia somo. Mwalimu wao ni zeruzeru (kutoka kundi linalotengwa na jamii).</p>	<p>Mvulana aliye chini kulia pichani inawezekana hafurahii somo, kakina.</p>	



*Wanasemina wakichunguza picha kujibu swalii:
"Elimu-jumuishi inaonekana je?"*

2.3. 'Elimu-jumuishi' ni mchakato endelevu

Picha inayo dadisi jibu la zoezi hapo juu inaonesha kuwa 'shule-jumuishi' haioneshwi kwa sura moja tu. 'Ujumuishi' shuleni ni matokeo ya mambo mbalimbali yakijumlishwa pamoja. Shule kamilifu kabisa haipo. Elimu-jumuishi ni dira au lengo ambalo ndilo tunatafuta wakati wote. Kwa kupitia mchakato wa mabadiliko na mageuzi tunaweza kufikia dira au lengo hili na kuwa 'jumuishi' zaidi. Aidha kila wakati kutakuwa na sababu mpya za watoto kutengwa - hii ni kwa sababu kuna mabadiliko ya mara kwa mara katika masuala yetu ya kisiasa, kijamii na kimazingira. Hivyo tunapaswa nasi kubadilika ili kukabiliana na sababu hizo mpya za kuwabagua watoto. Tunaweza kufanya mabadiliko makubwa katika mfumo mzima wa elimu, au mabadiliko madogo katika shule moja moja.


"Elimu-jumuishi ni kama kutengeneza gari jipya. Unaanza kutengeneza vifaa mbalimbali; halafu unavipangilia pamoja ili kulikamilisha gari; na kisha gari linaanza kutembea. Lakini utahitaji kulikarabati pale linapopata matatizo mapya ili uweze kuendelea kulumia".

(Mwanasemina)

Ili tuendelee na dira yetu ya 'elimu-jumuishi' ni lazima tujifunze kutoka miongoni mwetu. Tunalazimika kuona ni mageuzi gani makubwa na madogo wengine wameyafanya, ambayo tunaweza kujaribu kuyafanya katika sehemu zetu. Wakati mwingine pia tutatakiwa kurejea nyuma na kuona nini tulichokuwa tukifanya na kuwaomba watu wengine watafakari kazi yetu.

Wakati mwingine tunakwama tunapojaribu kufanya elimu-jumuishi. Ili kuukabili mkwano huo, tunapaswa **kuangalia** tulivyofanya huko nyuma. Tunapaswa pia **kuangalia** yanayoendelea kwa sasa, na kuona watu wengine wanafanya nini. Kisha tunatakiwa kuchambua taarifa tulizokusanya ili **kufikiria** namna itakayotusaidia kusonga mbele kwenye lengo letu la 'ujumuishi'. Na hatimaye **tunayafanya kwa vitendo** mawazo yote tuliyoyapata. Mara tunapokuwa tumeyafanyia kazi kwa vitendo, tunaangalia kwa makini matokeo yake na kuyatathmini, ili hatimaye

tunaweza kuboresha utendaji wetu zaidi na zaidi wakati ujao. Kwa kifupi, ni mchakato endelevu unaoakisi nyuma na kurekebisha ambao utatufanya tuendele mbele na dira yetu ya elimu-jumuishi.



Huu mchakato wa **tazama-tafakari-tenda** unaweza kutusaidia kuendelea kufanya marekebisho kuelekea elimu-jumuishi. Ni mchakato wa **Utafiti-kwa-Vitendo** (*action research*) – ambapo tunatafiti na kuchunguza hali ili tuweze kurekebisha bila ya kusubiri muda mrefu. Wakati mwingine ni kutumia busara tu. Siyo mchakato changamano au wa kutisha. Ni kama namna tunavyoishi maisha yetu ya kawaida – yaani tunaangalia yanayotutokea kila siku; tunatafakari namna ya kutatua na kuyafanya maisha yetu yawe bora zaidi; na kisha tunayafanyia kazi mawazo yetu kwa vitendo.³

Washiriki pia walihoji na kujadili kama *utafiti-kwa-vitendo* unaweza kufaa katika mbinu rasmi zaidi za mipango ya mradi kama zile za uchangunuzi wa *SWOT* (*strengths-ubora, weaknesses-udhaifu, opportunities-fursa, threats-vikwazo*) ambazo mara nyingi hutakiwa kufanywa na wafadhili. Mbinu zinazotumiwa katika *utafiti-kwa-vitendo* zinapatikana kwa watu wa ngazi za mwanzo kabisa katika jamii. Hii ina maana kuwa hawa ndiyo wanaoweza kukusaidia kukusanya na kuchambua aina ya data unazohitaji kufanyia uchambuzi wa *SWOT*. Kitu kizuri kuhusu utafiti huu siyo tu kukusaidia kukusanya data kwa ajili ya projekti au ripoti yako rasmi, bali unakusaidia kupata habari ambazo unaweza kuzitumia moja kwa moja kurekebisha kazi yako.

2.4. Elimu-jumuishi humaanisha *kuwepo, kushiriki na kunufaika*



'Elimu-jumuishi' haimaanishi kuongeza shuleni idadi ya watoto waliokuwa wametengwa. Patrick Kangwa na Edwina Mulenga Mumba walichangia kwa kusema kuwa watoto siyo *kuwepo* tu darasani, bali *washirikishwe* na *kunufaika* pia. Vipengele hivyo vitatu ni muhimu sana kuwepo kabla hatujadai kuwa na 'elimu-jumuishi'. Hakuna maana ya kuhangaika kuwatafuta watoto waliotengwa na kuwaleta shule (darasani) kama hawashirikishwi, na kama hawanufaiki au kupata chochote darasani.

³ Unaweza kusoma zaidi kuhusu mchakato wa 'tazama-tafakari-tenda' katika mwongozo wa *EENET: kujifunza kutokana na haki mbalimbali*. Kwa maelezo zaidi tazama orodha ya vitabu vilivyopendekezwa, ukurasa wa?

Watoto hushiriki katika maamuzi

Darasani lazima niwe karibu na wanafunzi; hivyo huwafanya wamudu kujifunza kwao. Tunachukua mfano wa watoto wanaopiga kelele darasani (kuongea ovyo, sauti ya usumbufu). Wanafunzi katika darasa langu walikuwa katika vikundi. Kila kikundi kilipewa daftari lake. Niliwauliza wanieleze maana ya 'kupiga-kelele'. Waliniorodheshea mambo 23 yaliyokuwa yakiwasumbua. Waliyaandika madaftarini.

Tulichunguza tatizo lingine. Tatizo la wanafunzi kuchelewa darasani. Wanafunzi waliamua kutafsiri maana ya 'uchelewaji na utoro'. Kila kikundi walikumbuka siku iliyokuwa na kelele darasani, uchelewaji na utoro katika kikundi chao. Hili lilikuwa zoezi la kuhakikisha kama wanafunzi wote wapo darasani. Lakini pia lilikuwa zoezi la kuhakikisha watoto wote wanashiriki kikamilifu katika maamuzi darasani na katika mchakato mzima wa kujifunza. Wanafunzi hawa walipoingia kidato cha 6 tuligundua kuwa walikuwa na uwezo zaidi wa kufanya kazi-mradi (projekti). Pia walikuwa na ufahamu mkubwa wa masuala kama vile *ulemavu* na *UKIMWI* ambapo ilikuwa ni matokeo ya kufanya uchunguzi na kufuatilia tabia na utoro miongoni mwa vijana. Mwalimu wao mwingine aliona wamefaulu vizuri katika mitihani, na hivyo aliwaacha peke yao darasani waendeleo kujusomea. Yote haya ni kwa sababu walikuwa wameshazoea kupeana majukumu kwa ajili ya nidhamu ya darasa lao.



Mifano ya madaftari ambayo wanafunzi walimokuwa wakirekodi tabia darasani

Pia katika kuhakikisha watoto wote wanashiriki darasani tulitumia **jozi** au **mapacha** (twinning). Kwa mfano mwanafunzi zeruzeru (aliyeoneshwa kwenye picha kipengele cha 2.2 nyuma) mwanzoni wenzake walikuwa wanamkimbia darasani kwa imani za ushirikina. Tulipompachaisha (twinning) na mwanafunzi mmoja kama pacha wake na rafiki yake wa kudumu, walianza kufanya kazi za darasani pamoja. Wanasaidiana hata nje ya darasa. Kwa sasa zeruzeru huyo anakubalika kwa wenzake, na ameingizwa kwenye jalada la darasa. Kufanya mapacha tunaangalia vigezo mbalimbali kama vile, nani anaishi karibu na nani; nani aliye sawa naye kiumri; na tunazingatia hali za awali zilizowahi kutokea au hata urafiki mpya unaoanza miongoni mwao, n.k. [Patrick Kangwa].

Jinsi mwalimu anavyohakikisha kuwepo, kushiriki na kunufaika kwa wanafunzi

Kwa *elimu-jumuishi*, unatakiwa kuzingatia mambo haya yote matatu badala ya kufikiria *kuwapo* kwa watoto darasani tu. Ni jinsi gani tutahakikisha kuwa wanafunzi wapo shuleni kila siku? Tunashirikiana na wazazi kuhakikisha kuwa watoto wanaruhusiwa kuja shule kila siku. Tunahakikisha kuwa kila mtoto anafika shuleni na tunamuondolea hisia au fikira ya kujisikia mnyonge (kama ni mlemavu). Tunatakiwa kumwelewa vizuri kila mtoto.

Kuhakikisha *ushirikishwaji* watoto wote, kila wakati tunajaribu kutafuta njia mbalimbali za kushirikiana na watoto. Tunatumia kazi za vikundi, na njia za ufundishaji/ujifunzaji zinazomzingatia mwanafunzi katika mchakato mzima wa kufundisha na kujifunza. Mwalimu anapaswa kuzungukia wanafunzi darasani, siyo kusimama mbele tu; na tunahakikisha kila mtoto anapewa nafasi ya kuzungumza (au kushiriki). Wanapozungumza na kujibizana wanafunzi, pia hufahamiana. Kunufaika au kupata maarifa mapya pia ni muhimu sana. Tunahakikisha njia za kufundishia zinafaa darasani. Tunamtazama kila mwanafunzi na kuwa huru kwake. Kama mazoezi tuliyoandaa hayaeleweki kwa wanafunzi, tunalazimika kuyatathmini na kurekebisha mkabala wetu wa ufundishaji. Tunampa kila mtoto nafasi ya kujibu tukianza na wale wasioelewa vizuri badala ya kuchagua wale wenye uwezo tu. Tunawapa nafasi ya kujieleza na kujibu (wasio na uwezo mkubwa) ili kuhakikisha kuwa wote darasani *wananufaika* na kinachofundishwa. [Edwina Mulenga Mumba].

Kushiriki na kunufaika kwa wasioona

Kuna maoni mbalimbali kuhusu dhana ya *ujumuishi* kwa wanafunzi wasioona. Wanasemina walijadili suala la wanafunzi wasioona ambao wanahitaji mashine ya kuchapa (*braille*) ili waweze kushiriki na kunufaika au kupata maarifa mapya darasani. Kutokana na mifano ya hapo juu, walimu wanapaswa kuzungumza na wazazi na kuwaeleza uwezo wao kwa wanafunzi hao. Wanaweza kufundisha kwa njia zisizotumia mashine za kuchapa na kuwasaidia wasioona kupata marafiki darasani ambao watawasaidia kusoma na kuandika mazoezi. Ilipendekezwa kwamba, kwa kuwa *elimu-jumuishi* ni mchakato hatuwezi kupata kila kitu kwa mara moja. Tutahitaji kuamua kati ya haya mawili: (i) Je, ni bora mtoto asiyeona aendelee kubakia nyumbani bila kupata elimu mpaka vifaa sahihi vitakapopatikana? (ambapo vinaweza kuchukua muda mrefu). (ii) Au, je ni bora mtoto huyo aanze kwenda shule hata kama vifaa havijapatikani kwanza? Kumbuka mtoto ana haki ya kupata elimu. Ufumbuzi wa mahitaji yake unaweza kupatikana kadri unavyoendelea. Na kwa kumpeleka mtoto huyo shule siyo tu ni changamoto kwa wazazi wake, bali pia ni kwa jamii nzima inayoizunguka shule.

Kiribati katika kisiwa cha Pasifiki (Pacific), walimu wamebuni njia za kuwasaidia wasioona kujifunza *Braille* bila hata ya kuwa na vifaa vya kufaa. Shule moja hutumia mayai katika boksi la mayai kuwafundisha *nukta-sita* ambazo ndizo msingi wa mashine ya kuchapa ya *braille*. Hii ni njia nyepesi na rahisi kama vifaa rasmi vya *braille* havijapatikana.



Zana ya kienyeji ya kufundishia 'braille'

Hata hivyo watu wengi hufikiri kuwa haitoshi kupeleka shule mtoto asiyeona bila huduma maalum. Siyo vyema kumwacha aketi darasani kusikiliza tu. Na kwamba ni vigumu kwa mwalimu asiye na ujuzi wala stadi za kufundisha wasioona kuamua kumfundisha mtoto huyo. Hii ilileta hoja ya kuwa na shule maalum kwa ajili ya *elimu-jumuishi* ili pale ambapo kuna wenye ujuzi na vifaa maalum paendelezwe zaidi na kurasmishwa na kuwa *shule-jumuishi*.

3. Vikwazo na ufumbuzi wake

3.1. Kubainisha vikwazo vya ujumuishi' na wanaoathiriwa navyo

Kuna sababu nyingi kwa nini baadhi ya makundi ya watoto hawapati haki yao ya elimu bora wanayostahili. Hii ni kwa sababu kuna aina mbalimbali za vikwazo dhidi ya *elimu-jumuishi*. Mara nyingi tunaangalia rasilimali na vifaa vya kuonekana (kama vile uhaba wa fedha, n.k.) kwa sababu hivi ni rahisi kuonekana. Hata hivyo kuna vikwazo vingine ambavyo ni sawa na hivyo lakini tunaweza kuvitatua kwa urahisi kabisa.

Hata hivyo vikwazo vya *elimu-jumuishi* vinaweza kuwekwa katika kategoria zifuatazo:

- **Vikwazo vya kimazingira:** mf, majengo ya shule na vyoo ambavyo si rahisi kufikika.
- **Vikwazo vya mwelekeo wa tabia:** mfano tabia ya woga, aibu, kukata tamaa, n.k.
- **Vikwazo vya sera:** mfano ratiba za shule kubanwa sana, kutotumia lugha-mama au Lugha ya Taifa kufundishia, n.k.
- **Vikwazo vya kiutendaji na ujuzi:** mfano kutotumia njia-shirikishi katika ufundishaji, n.k.
- **Vikwazo vya rasilimali:** mfano uhaba wa walimu, wingi wa wanafunzi katika darasa, n.k.

Wanasemina walifanya mazoezi ya vikundi kwa kuangalia picha mbalimbali za shule kutoka Zambia na Indonesia. Waliambiwa kuchunguza vikwazo mbalimbali kwenye picha hizo – vikwazo vya wazi na visivyoonekana kwa urahisi (na visiwe vile vya rasilimali na mazingira tu)⁴. Katika majadiliano ya wote, waliorodhesha vikwazo vyote walivyobainisha kwenye makundi yao. Kisha walieleza aina y vikwazo hivyo na nani walioathirika navyo. Ikuatayo ni mifano michache (muda haukatosha kujadili kila kikwazo kwa kina):

Kikwazo	Aina ya kikwazo	Anayeathirika
Mabonde, milima kwenye eneo la shule.	Mazingira	Watoto walemavu na walimu wazee
Hakuna madarasa karibu	Rasilimali	
Upweke (mtu anaonekana mpweke)	Mwenendo/tabia	
Choo hakifikiki	Mazingira	Watoto walemavu
Walimu hawajali	Mwenendo/tabia	Wanafunzi, wazazi, wizara, jamii.
Ofisi ya walimu ni ndogo	Mazingira/sera	Walimu

⁴ Taswira mbalimbali zilitumika ambazo hatuwezi kuziwasilisha hapa. Zote zinapatikana kwenye CD-ROM kutoka *EENET* kwa watu wanaopendelea kuzitumia.

Kikwazo	Aina ya kikwazo	Anayeathirika
Wanafunzi wanateka maji muda wa shule.	Mwenendo/tabia	Wanafunzi wote (mara nyingi wasichana).
Mlango mfinyu, dirisha dogo	Mazingira	Walimu, wanafunzi
Shuleni ni mbali sana	Mazingira	Walimu, wanafunzi, wazazi – walemavu na wadogo, wagonjwa, na wenye njaa.
Msichana ananyanyaswa na mwanamme-(kumbuka hii ilikuwa picha ya kwenye bango, siyo halisi iliyopigwa)	Mwenendo/tabia	Wasichana
Muundo wa eneo/majengo ya shule.	Sera	Walimu, wanafunzi na wazazi (walemavu na wasio walemavu).
Watoto sokoni/kazi ya watoto (kufanyishwa kazi)	Mwenendo/tabia, rasilimali	Wanafunzi – hususan wale walio fakiri majumbani kwao.

Kila kikwazo cha ‘Elimu-jumuishi’ kwa kawaida kinaathiri zaidi ya kikundi kimoja cha watu. Kama tukiweza kutatua kikwazo kimoja tunakuwa tumesaidia kundi kubwa la watoto kuingia katika mfumo wa ujumuishi, kwa mfano walemavu.

Viashiria mchanganyiko

Although most participants work specifically with disabled people and for disability organisations, they were advised not to limit themselves only to thinking about disability-related barriers. Participants therefore brainstormed all the different identities that a disabled person could have, in addition to being considered disabled, e.g.:

- mtoto/umri
- msichana/mvulana
- utaifa/kabila/lugha
- dini
- ukoo/kizazi
- mjini/shambani (kijijini)
- kuwa/kutokuwa na uwezo wa akili
- muonekano wake(haiba)
- kuathirika/kuambukizwa na UKIMWI
- yatima
- kazi
- uwezo wa kiuchumi, n.k.

Orodha hii inaonesha mchangamano wa watu. Hatuwezi kuwaona watu kama walemavu tu; bali wanaweza kuwa na matatizo mengine juu ya ulemavu wao. Msichana mlemavu kwa mfano, anaweza kukabiliwa na kikwazo cha kutothaminiwa au kutengwa kwa sababu ya jinsia yake tu na siyo ulemavu alio nao. Hivyo wale wote wanaojishughulisha na walemavu na mashirika yake wanapaswa kuzingatia masuala yote haya yanayosababisha kutengwa au kutothaminiwa kwa watoto katika jamii.

Wadau ni akina nani?

Tumekuwa tukitumia neno “wadau” mara nyingi sana, lakini ni vizuri tuchunguze maana yake halisi. Wanasemina walilitafsiri kuwa “ni kila mtu anayechangia kufanyika kwa jambo fulani”. Waliorodhesha mifano ifuatayo kama wadau:

- wazazi
- watoto
- walimu
- wanasiasa/viongozi
- serikali
- mashirika yasiyo ya kiserikali/washirika
- wafadhili
- yeyote anayejisikia kusaidia
- wafanyabiashara/sekta binafsi
- vikundi/mashirika ya kidini, n.k.

3.2. Ufumbuzi wa vikwazo/matatizo

Kila mazingira (shule, wilaya, nchi, n.k.) yana namna ya pekee, na hivyo hata changamoto nazo kuelekea ‘ujumuishi’ zitafautiana sehemu na sehemu. Utatuzi na ufumbuzi wa vikwazo na matatizo utategemeana zaidi na maarifa pamoja na uzoefu wa sehemu hiyo. Ufumbuzi utakaokusaidia kuwaingiza katika ‘elimu-jumuishi’ watoto waliotengwa wa sehemu fulani unaweza usisaidie katika sehemu nyingine. Ni muhimu sana kujifunza kutoka kwa wenzetu njia mbalimbali zilizosaidia na ambazo hazikufaa kabisa; ili tuweze kuzitumia kwa umahiri zaidi katika sehemu zetu. Tukichukua njia fulani kutoka kwa uwenzetu na kuitumia bila kuihusisha na mazingira halisi ya kwetu, inaweza isifanye kazi kabisa – na hii inaweza kuwafanya watu waghafilike na kuhisi kuwa ‘elimu-jumuishi’ ni mchakato usiowezekana!

3.3. Wanasemina walitaja vikwazo na ufumbuzi gani?


Wakati wote wa warsha wanasemina walipewa mazoezi mbalimbali ya kuwasaidia kuona na kujadili matatizo au vikwazo halisi vya ‘ujumuishi’ katika elimu (na kisha kujadili ufumbuzi ambao ungepaswa kujaribiwa au kufanywa). Mazoezi-shirikishi yaliyotumika hasa ni pamoja na kuchora kielelezo vya mlima, uzoefu binafsi na kuandika, na kuchunguza shule zilizotembelewa (ziara mashuleni kwa nia ya uchunguzi). Njia zilizotumika katika mazoezi haya zimejadiliwa kwa kina katika ripoti ndogo.

‘Zoezi’ la kielelezo cha mlima kinawasaidia washiriki kufikiri; *nini wanatafuta* (lengo la kufika kileleni); *vikwazo wanavyokabiliana navyo* kabla ya kufika kileleni; na *dalili za mutumaini* ambazo wameshazipata safarini au mawazo waliyonayo kuhusu ufumbuzi wa vikwazo hivyo. Hii ni njia bora kuliko majadiliano ya kawaida. Ili kuwafanya wanasemina washiriki na kuchangia kikamilifu kutokana na kielelezo hicho cha mlima, tulitumia njia ya maigizo ya mkutano wa wanahabari. ‘Uzoefu-binafsi na kuandika’ unawasaidia washiriki kufikiria suala moja kwa kina (kikwazo au mfano wa ufumbuzi wake). Wengine wanaweza kujadili na kuunganisha mawazo yao waliyoandika na kuunda habari ya kikwazo na ufumbuzi wake katika sehemu zao.

'Uchunguzi wa mazingira' ya maisha halisi (kwa mfano; shuleni na madarasani) unawafanya washiriki kujifunza namna wengine wanavyofanya, na kujaribu kuhusisha na hali halisi ya sehemu zao kama wanatofautiana au la.

Ufuatao ni ufupisho wa vikwazo mbalimbali vya 'ujumuishi' katika elimu, na mawazo mbalimbali ya ufumbuzi wa vikwazo hivyo katika kila nchi. Ufupisho huo umetokana na majadiliano ya vielelezo vya mlima, maigizo, na maandishi ya washiriki, na pia kutokana na kazi rasmi zilizokuwa zikiwasilishwa na wanasemina wakati wa warsha.

Elimu-jumuishi: vikwazo na ufumbuzi wake Tanzania



Vikwazo	Ufumbuzi (halisi /mapendekezo)
<p>Kutoelewa chochote kuhusu 'elimu-jumuishi' na kuwa na mwelekeo hasi kuhusu 'ujumuishi' katika elimu.</p>	<p>Fanya mikutano kuhusu kuelimishana na kuhamasishana kuhusu mfumo huo wa elimu (tangu watu wa serikalini mpaka kwa wale wa kawaida vijijini). Tumia mifano kutoka nchi nyingine kuelezanamua 'elimu-jumuishi' inavyofanya kazi.</p> <p>Kubadili mwelekeo wao katika ngazi ya wilaya, shirikiana na mashirika yasiyo ya serikali yenye mwelekeo chanya katika 'ujumuishi' ili kwa pamoja muwafahamisha suala hili maafisa mipango wa wilaya ili waweze kuingiza mikakati ya 'elimu-jumuishi' katika mipango ya wilaya.</p> <p>Kubadili mwelekeo wa watoto – uelewa na hamasa vijengwe kwa kuzingatia shule na jumuiya yake.</p> <p>Serikali inaandaa sera ya kuanzisha 'elimu-jumuishi' kitaifa. Hii itasaidia sana kuhamasisha na kuendeleza kazi kisheria kwa shule na wazazi.</p>
<p>Uhaba wa walimu wa 'elimu-jumuishi' na watoto wenye mahitaji maalum (walemavu). Ukosefu wa wataalam katika mfumo wa elimu</p>	<p>Program ya mafunzo inaendelea. Kwa sasa walimu wakuu huchagua walimu wenye moyo na wanaopendelea kufundisha watoto wenye ulemavu.</p> <p>Mtaala wa elimu unapitiwa kwa sasa ili kila mwalimu anayeenda chuoni aweze kufundishwa kuhusu 'elimu-jumuishi'.</p> <p>Kuhakikisha mafunzo yanayotolewa, tutatumia mifano ya watu wazima wenye ulemavu kuelezea uzoefu wao tangu makuzi, elimu, n.k. Wakaguzi wa shule na walimu wakuu hao watapewa mafunzo huku walimu wakuu wakijadili na kubadilishana uzoefu.</p> <p>Yafuatayo pia yangefaa kujaribiwa:</p> <ul style="list-style-type: none"> • semina nyingi zitolewe kwa walimu, wakaguzi na maafisa wa serikali za mitaa – na wawape wenzao mashuleni kile walichojifunza • walimu wafanye ziara kwenye mashirika yanayoshughulikia watoto wasiojiweza/wenye ulemavu na shule maalum • serikali iwadhamini walimu wote wenye nia ya kutaka kusoma zaidi.
<p>Tafsiri mbalimbali za sera: Tanzania ina sera ya elimu na mafunzo ambayo inadokeza tu 'ujumuishi' katika elimu; inaeleza kwamba elimu ni haki ya watoto wote pamoja na</p>	<p>Wapanga sera (viongozi) wanatakiwa kuandaa miongozo ya sera ambayo itafafanua na kutoa majukumu kwa wahusika kuhusu 'elimu-jumuishi' (mf. kaya/wazazi au walezi, jamii, na serikali za mitaa - kwa kutumia idara zake kwa pamoja).</p> <p>Miongozo hiyo inatakiwa ieleze wazi majukumu ya</p>

<p>wale wenye ulemavu. Hata hivyo haikutaja wazi 'elimu-jumuishi' na hivyo uamuzi wa kuingiza watoto hawa unategemea jinsi watekelezaji wa sera hii watakvoyoitafsiri.</p>	<p>Serikali Kuu (wizara) katika kusaidia halmashauri na shule. Inatakiwa ioneshe majukumu ya shule, walimu, vyuo vya mafunzo, jumuiya za jamii, na mashirika ya watu walemavu.</p> <p>Kunatakiwa kuwekwe sheria ya "Elimu ni lazima na haki ya wote (pamoja na walemavu)" hii itatolewa kama sheria ya Elimu.</p> <p>Baadaye mwongozo wa sera na sheria ya Elimu vitatakiwa kutafisiriwa katika lugha ya wananchi na kutumiwa na wadau wote.</p>
--	--

TAMH (Chama cha wenye mtindio wa akili Tanzania) kimekuwa kikijitahidi kukabiliana na changamoto kadhaa za kuingiza 'ujumuisho' katika elimu. Hii ni pamoja na:


- Kuishauri Wizara ya Elimu na Utamaduni kukubali mradi wa Chama cha TAMH unaohusu 'Elimu-jumuishi' katika shule za Msingi. Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo na unafadhiliwa na 'Operation Day's Work/NFU' kutoka Norway. Mradi huo unafanyiwa majaribio katika kila wilaya – kinondoni, Mkuranga, Morogoro Vijijini na Iringa Vijijini.
- Mafunzo ya msingi/mwanzo ili kuelewa mahitaji na majukumu ya wadau muhimu.
- Kuendesha mikutano na Warsha katika wilaya hizo, mashule na jamii kuhusu 'elimu-ujumuishi'. Yote haya yanafanyika ili kuboresha mradi na kuendeleza; na pia kuwahamasisha wazazi kuleta watoto wao walemavu shuleni badala ya kuendelea kuwaficha majumbani.
- Kutengeneza na kusambaza matangazo (kwa mfano fulana, mabango, vijarida, makala, n.k.)
- Kuandika mwongozo wa mafunzo ya walimu-kazini katika shule za majaribio.
- Mafunzo ya walimu-kazini yameshafikisha walimu 142 na wakufunzi wa vyuo. Mafunzo yatolewayo yanajumuisha masuala ya mahitaji maalum ya watoto walemavu, elimu-jumuishi, kuchunguza aina mbalimbali za ulemavu, njia za kufundishia/kujifunzia, mtaala na kuboresha mazingira ya kujifunza, na jinsi ya kupata msaada kutoka serikalini/jamii/mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Mafunzo ya lugha ya ishara mpaka sasa yameshafikia walimu 20 kutoka wilaya 2 za majaribio. Mafunzo haya yalikusudiwa kuwawezesha walimu kuwasiliana zaidi na watoto wasiosikia, na vilevile kuwawezesha walimu kufundisha lugha ya ishara kwa watoto hao. Yaliendeshwa na Chama cha Wasiosikia Tanzania.
- Warsha kuhusu mipango ya 'elimu-jumuishi' katika shule ilifanywa katika kila wilaya ikishirikisha washiriki 80. Warsha hizi zililenga kuelewa vizuri masuala ya 'elimu-jumuishi'; kujadili matatizo katika kujifunza na jinsi ya kuyatatua, na kuanzisha vyombo vya usimamizi na tathmini. Washiriki walikuwa watu wote wenye majukumu ya kuandaa mipango ya muda mfupi na muda mrefu katika kiwango cha shule na wilaya.
- Mradi wa Maendeleo ya Vijana unakamilishana na mradi wa 'Elimu-jumuishi' kwa kuwahamasisha na kuwafundisha vijana wenye ulemavu stadi za maisha/jamii, kujitambua/kujiamini na stadi za ufundi. Kwa sasa imefikia wanafunzi 50 kutoka shule 7. Kambi mbili za vijana pia zimeshaanzishwa kuwawezesha mafunzo ya stadi za maisha/jamii na kuanzisha /kuendeleza moyo

wa kujitambua na kujiamini kwa kujitegemea na kushiriki katika michezo na burudani mbalimbali.

Jeshi la Wokovu Tanzania lilianzisha programu za 'elimu-jumuishi' katika shule za majaribio mikoa ifuatayo: Dar-es- Salaam (2000), Mbeya (2001) na Tabora (2002). Programu hizo zilijikita hususan katika 'ujumuishi' wa wanafunzi walemavu. Mikakati ifuatayo ndiyo waliyotumia kuweza kuingiza wanafunzi walemavu wengi zaidi mashuleni:

- Kuhusisha ukarabati wa shule husika. Huduma za ukarabati zilienda sambamba na kuangalia mahitaji ya watoto hao, kutoa vifaa vinauyohitajika na zana-saidizi za walemavu, na kuwagharia/kuwapeleka hospotali kwa msaada zaidi.
- Kuboresha zanambinu/mazingira ya shule kwa msaada wa Wizara ya Elimu na wafadhili kutoka nchi za nje. Hata hivyo shule mpya zinazidi kujengwa pasipo kuzingatia kuwepo/upatikanaji wa mazingira/vifaa muhimu. Jeshi la uokovu linajaribu kuihamasisha serikali kuweka sera itakayokazia ubora wa mazingira na kuwepo kwa vifaa na vifaa-saidizi kabla ya ujenzi kufanyika.
- Kuendesha warsha kuhusu 'elimu-jumuishi' kwa walimu 145 na kuandaa mwongozo wa mafunzo.

Elimu-jumuishi: vikwazo na ufumbuzi wake Lesotho



Vikwazo	Ufumbuzi (halisi au mapendekezo)
Hakukuwa na picha kamili ya kilichokuwa kinatendeka kuhusiana na ujumuisho katika elimu.	Mafunzo ya msingi/uchambuzi wa mazingira ulitolewa kuhusiana na 'elimu-jumuishi'. Hii ilifanyika baada ya projekti kuanzishwa (siyo kabla). Hii ilisaidia kwani kutokana na tathmini iliyokuwa imeshafanywa kulikuwa na mapengo ya ufahamu wa hali halisi ambayo yalihatiji kuzibwa.
Usafiri(Lesotho ni nchi ya vijiji na milima)	Bado hakuna ufumbuzi kwa hilo; mpaka labda kuwaomba wafadhili kutoa pesa za kuboresha mfumo wa usafiri na barabara. Shule nyingi zinajengwa ili kuwaondolea watoto usumbufu wa kusafiri kutoka kijiji kimoja hadi kingine. Hii inaweza kuwa changamoto pia kwa jumuiya nzima - kwani wanaweza kuwajibika katika kutatua matatizo ya usafiri wa kwenda shule.
Kutokuwa na kumbukumbu za kutosha.	Hatua zinachukuliwa na mwalimu na mwalimu mkuu kuhakikisha kuwa rekodi za mwanafunzi zinatunzwa ipasavyo hata kama mwalimu mhusika hayupo ama kahamishwa shule.
Janga la UKIMWI limeongeza idadi ya watoto wenye matatizo; hata hivyo siyo walimu wote walio na utayari wa kusaidia watoto walioathirika au kuambukizwa HIV/UKIMWI.	Suala hili lilitolewa Lesotho, lakini ufumbuzi wake haukujadiliwa kwa sasa.


Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Lesotho (MOET) ina sera ya *ujumuishi* wa watoto wenye ulemavu shule za kawaida za serikali katika viwango vyote vya elimu. Serikali ilikiri kuwa moja ya vikwazo vikubwa vya 'elimu-jumuishi' ni walimu kutokuwa na utayari au maandalizi mazuri ya kufundisha watoto zaidi ya wale wenye uwezo wa wastani na kuendelea. Wizara mara moja iliona kuwa ili 'elimu-jumuishi' ifanikiwe nchini, kuna haja ya kuboresha mafunzo ya walimu.

Kozi iliyokamilisha elimu ya mahitaji maalum na elimu-jumuishi ilianzishwa katika Chuo cha Elimu Lesotho mwaka 1995, lakini haikufanikiwa kwa kukosa wataalam wa kuendesha kozi hiyo. Katika mwaka 2004 Wizara ilimpeleka afisa mmoja kutoka kitengo cha Elimu Maalum ili akasaidie kuendesha kazi, na tangu hapo kuna maendeleo mazuri. (Kitengo cha Elimu Maalum ni programu katika Wizara ya Elimu na Mafunzo iliyoanzishwa mwaka 1991). Chuo hicho pia kinaboresha mafunzo ya walimu walemavu kwa kutoa chumba maalum, vifaa husika, mfasiri, n.k. Aidha Chuo Kikuu cha Lesotho kinaanza kutoa kozi za *elimu maalum* na *elimu-jumuishi* mwezi Agosti 2006.

Wizara ya Elimu na Mafunzo imefanikiwa kufanya yafuatayo ili kubadili mwelekeo wa 'ujumuishi' wa wanafunzi wenye mahitaji maalum/walemavu:

- Kutoa mafunzo kuhusu masuala ya 'Elimu maalum' kwa walimu, maafisa-Elimu na walimu wa vituo wilayani. Mafunzo haya yanahusu: kuwatambua watoto hawa, mifumo ya rufaa/kupeleka wenye matatizo hospitali, mipango ya Elimu kwa mtoto mmoja mmoja, na stadi za ushauri-nasaha.
- Kutembelea shule ili kuangalia na kusimamia maendeleo ya wanafunzi hawa. Kuna utaratibu wa walimu wakongwe wanaosaidia katika 'elimu-jumuishi'. Mfumo huu unasaidia walimu kuwatambua, kuona na kuwapangia mmoja mmoja mipango ya elimu. Aidha, mfumo huo unasaidia katatua matatizo katika utekelezaji wa 'elimu-jumuishi', na pale inapohitajika warsha/semina inafanyika moja kwa moja bila kusubiri.
- Kuwahamasisha wananchi juu elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ya Elimu (walemavu) kwa kuitisha mikutano ya hadhara na kusheherekea sikukuu za kimataifa za ulemavu na/au watu wasiojiweza.
- Kushirikiana na idara zingine za Wizara ya Elimu na Mafunzo, wizara zingine, wadau wa elimu, na mashirika yasiyo ya kiserikali kuhusiana na masuala ya ulemavu au watoto wasiojiweza.

Elimu-jumuishi: vikwazo na ufumbuzi wake Uganda



Vikwazo	Ufumbuzi (halisi au mapendekezo)
<p>Utoro – kwa walimu na wanafunzi</p>	<p>Kuhusu utoro kwa walimu, kozi za mafunzo kazini ndio suluhu. Walimu wakiuona ualimu ni kazi nzuri, watapenda kuja kazini.</p> <p>Kuhusu utoro wa wanafunzi, kama watoto wanaona wanashirikishwa shuleni, hawatoroki ovyo.</p> <p>Tunaweza kuwaita wazazi na kuwaomba wawahimize watoto kuja shule, na wazazi kushiriki katika maisha ya kila siku ya shule.</p> <p>Tunaweza kuyafanya mazingira ya shule yawe ya kufurahisha na karimu – hivyo watoto lazima watakuja shule.</p> <p>Utoro unategemeana na jamii pia kwa sababu wasichana na wavulana hufuatana na wazazi sokoni au huamua kukaa nyumbani bila sababu za msingi. Inabidi kuwahusisha viongozi wa serikali za mitaa na kuwaomba maafisa wa masoko kuwapiga marufuku wanafunzi kuonekana sokoni.</p> <p>Wakati mwingine utoro husababishwa na uzembe wa uongozi wa mwalimu mkuu. Kwa hiyo wakaguzi wa shule wanapaswa kuwachunguza kikamilifu wakuu wa shule.</p>
<p>Uchache wa zanambinu mashuleni (madarasa machache mno, samani chache, idadi ndogo ya walimu husika, n.k.)</p>	<p>Serikali iwahamashe zaidi wazazi na jamii nzima kuchangia katika kukamilisha ujenzi wa madarasa au kuchangia kwa kujitolea nguvu zao au kutoa vifaa katika projekti za majengo ya shule.</p> <p>Serikali iziruhusu wilaya kuweka sheria ndogo ndogo za kuwashirikisha wanajamii katika ujenzi wa majengo shuleni.</p>


<p>Mwelekeo hasi (mbaya) wa jamii</p>	<p>Ufumbuzi sio tu kuwashawishi wazazi kupeleka watoto wao shuleni, bali pia kuwaeleza wanajamii kuwa watoto wanahitaji elimu, na ni jukumu lao (jamii) kuchangia katika elimu.</p> <p>Uongozi wa shule na viongozi wa serikali/kidini wanapaswa kusaidia kuweka wazi dhana nzima ya <i>elimu-jumuishi</i>.</p> <p>Watoto wapewe makabrasha (<i>pamphlets</i>) yaliyoandikwa kwa lugha za kienyeji (kikabila) ili kuwasomea wazazi wao, na mabango pia yawekwe katika sehemu tete za jamii.</p> <p>Kutafuta mifano au walimu wenye ulemavu ambao wanaweza kuzungumzia 'elimu-jumuishi' kwa watoto shuleni.</p> <p>Tunaunda kamati za shule – kamati za walemavu na jamii.</p> <p>Tunahitaji wazazi kushirikiana na kufanya kazi kama timu moja kuhamasisha 'ujumuishi' mashuleni, kwa mfano kuwapa mifano ya walemavu waliofanikiwa, kutumia programu zinazojikita katika jamii kuwasaidai hawa wasojiweza, na kuunda vikundi vya wazazi ambao wanasaidiana.</p>
---------------------------------------	--

Katika kuongeza mwamko na kuondoa utata uliokuwepo kati ya dhana ya 'elimu ya maalum' na *elimu-jumuishi*, kipindi cha mazungumzo kwa radio kiliandaliwa. Kipindi hiki kilisikika kwa lugha ya wenyeji hadi wilaya ya Busia. Wananchi waliruhusiwa kupiga simu wakati wa kipindi.

Timu ya wataalam iliandaliwa. Hii ilihusisha Mkuu wa Kitivo cha Elimu Maalum Idara ya Elimu Chuo Kikuu cha Kyambogo; Mkaguzi wa Shule wa Wilaya ya Busia; mwalimu wa mazoezi ya 'elimu-jumuishi'; afisa-maendeleo ya jamii; na afisa-elimu wa wilaya. Majadiliano yalihusu: fasili ya '*elimu-jumuishi*' na uhusiano wake na Elimu ya Msingi kwa Wote; ushirikishwaji wa jamii katika kuboresha elimu-jumuishi; na namna ya kumshughulikia mtoto aliyebaguliwa ama kutengwa na wenzie katika darasa la kawaida.

Simu zilizokuwa zikipigwa wakati wa kipindi/programu zilishirikisha watu kutoka hata nje ya wilaya, na maoni yao kwa ujumla yalionesha kuwa kipindi kilisaidia sana kuelezea maana halisi ya 'elimu-jumuishi'. Kipindi cha redio kilisaidia kutayarisha mazingira ya warsha itakayowashirikisha walimu na walimu wakuu.

Elimu-jumuishi: vikwazo na ufumbuzi wake Kenya




Vikwazo	Ufumbuzi (halisi au mapendekezo)
Ukosefu wa mfumo mzuri wa stadi za mawasiliano	Tunahitaji zaidi lugha ya ishara, breili, na stadi za mawasiliano kwa jumla. Tunaweza kuwashirikisha wazazi wa watoto walemavu , mfano; kuwapa mafunzo ya lugha ya ishara, n.k. Walimu na wazazi wengi hawana stadi za breili, na tunaweza kusaidia jamii kujifunza angalau mambo ya msingi ili nao waweze kuwasaidia watoto wao mapema kabisa.

<p>Sera na kazi halisi haviendani (vinapishana)</p>	<p>Kuna sera tayari ambazo zinaeleza masuala ya <i>elimu na ujumuishi katika elimu</i> lakini hali halisi ni kinyume. Hii ni kwa sababu ya ugumu wa mtaala kutokubaliana na sera hizo za ‘ujumuishi’. Tunahitaji kubadili mfumo wa kulenga mtihani, na kuwaongezea maslahi walimu ili wafanye kazi kwa manufaa ya watoto wote.</p> <p>Tunatumia makundi ya kutusaidia kuchunguza matumizi au utekelezaji wa sera – wanaweza kuona hata zaidi ya NGO (mashirika yasiyo ya serikali) yanavyoweza.</p>
<p>Mwelekeo hasi wa wazazi, walimu, watoto, n.k.</p>	<p>Baadhi ya wazazi bado wanaona aibu au wanashikilia miiko na mila za jadi. Si rahisi kueleza bayana kuwa wana watoto hawa. Tunahitaji kuwa na vikundi vya wazazi, wazee wa kanisa, n.k. ambao wanaweza kurejesha mwelekeo chanya kwa jamii.</p> <p>Ili kufaulu katika hili, kunapaswa kufanywa mikutano kujadili masuala ya ‘ujumuishi’ na kufuatiwa na warsha, semina, n.k. kwa kuwashirikisha pia viongozi wa kidini, katika mikutano ya viongozi wa mitaa, n.k.</p> <p>Tunaweza pia kusaidia kuunda uongozi miongoni mwa wazazi ili waweze kueneza taarifa kwa urahisi.</p>
<p>Uhaba wa vifaa/rasilimali (watu na vitu)</p>	<p>Tunafanya kazi kwa kushirikiana na wazazi, vikundi na mashirika yasiyo ya kiserikali kuona kama tunaweza kupata vifaa.</p> <p>Hakuna walimu wa kutosha wenye sifa. Tuna programu za Elimu Kazini kwenye ngazi za msingi, na tunawapeleka walimu kwenye baadhi ya taasisi za mafunzo kwa programu za kozi fupi fupi. Kwa hiyo katika muda mfupi ujao tutakuwa na walimu wa kutosha wenye sifa na stadi zinazostahili.</p> <p>Tunawasiliana pia na vikundi vya walemavu kuhusu jinsi ya kutengeneza zana za kufundishia kwa kutumia vifaa vya kienyeji.</p> <p>Kwa kuwa sera huchukua muda, na mafunzo pia huchukua muda. Hatuwezi kusubiri tu hadi serikali itoe mafunzo haya kwa wahitimu wa sekondari tunasaidia kuharakisha mchakato huu kwa kuwachukua walimu wazoefu kuhudhuria mafunzo haya japo kwa programu fupifupi. Walimu hawa baadae huwa wakufunzi wa wakufunzi (<i>trainers-of-trainers</i>), na mchakato mzima unazidi kupanuka.</p>

Elimu-jumuishi: vikwazo na ufumbuzi wake Nepali na Palestina


Kuwa kuwa nchi hizi ziliwakilishwa na mshiriki mmoja mmoja kwenye warsha, washiriki hawa walishirikiana kujadili vikwazo na ufumbuzi wake. Pamoja na nchi hizo kutofuutiana, bado kuna maeneo ambayo yalifanana.



Vikwazo	Ufumbuzi (halisi au mapendekezo)
Matatizo ya usafiri wa kwenda shuleni	Nchini Palestina, maeneo ya tahadhari yanawazuia watoto kutoenda skuli zilizo karibu. Shule nyingi zipo jirani ya Israeli na hivyo ni tatizo. Tunaweza kuwahamishia walimu shule ambazo watoto wanafika bila mashaka. Tunaweza pia kujenga shule karibu na maeneo ya tahadhari - ingawa bado ni tatizo kukitokea machafuko.
Umasikini na ujinga katika jamii.	Nchini Nepali, <i>Mtandao wa NFU</i> wa Nepali ni kikundi cha wazazi. Watu masikini (fakiri) wenye watoto walemavu hushindwa kuwapeleka kwa mganga/muuguzi, na familia (au waume) zao hawana msaada wowote. Kwa hiyo ufumbuzi ni kuwa na programu za mazungumzo ya wazazi-kwa-wazazi ili

	<p>kusaidia kutatua matatizo hayo. Tumeanza programu hizo.</p> <p>Nchini Palestina (kuhusiana na umasikini), Wizara ya Elimu inapanga jinsi ya kuushughulikia. Kila mwanafunzi analipia kwenda shule, lakini kama hana fedha anasaidiwa bure. Kuna mahusiano mema na jamii – tunakubaliana nao - kisha wanachangia mali na vifaa.</p>
<p>Sera isiyo sadifu wala kuendana</p>	<p>Nchini Palestina, tulipofanya uchunguzi wa kuwa na ‘elimu-jumuishi’ katika jamii, tuligundua kuwa watoto walemavu wengi walikuwa shuleni tayari. Tuliambia kuwaambia wapanga sera, na walikubali kuingiza ‘elimu-jumuishi’ katika shule zote za serikali.</p> <p>Nchini Nepali, tuna shule maalum kama vituo vya watoto (<i>day-care centres</i>). Wazazi hawapendi watoto kwenda shule za kawaida, wana penda ‘shule maalum’. Serikali imeanzisha <i>elimu-jumuishi</i> katika baadhi ya vitengo/maeneo. Wanaita ni ‘elimu-jumuishi’, lakini kusema kweli, siyo. Walimu wa shule za kawaida hawafundishwi; tunajitahidi sana kuishawishi serikali; na sasa bado tunapigania sera.</p> <p>Tunajitahidi kupata taarifa duniani kote ili kutusaidia kuishawishi serikali. Mwezi Machi/Aprili 2006 tutakuwa na mkutano mkubwa kama sehemu ya kazi yetu ya kuishawishi serikali.</p>
<p>Mwelekeo hasi wa walimu na ukosefu wa ujuzi/maarifa kujiamini Kuhusu kufundisha watoto walemavu</p>	<p>Nchini Palestina, tunaunda Kamati Maalum ya wajumbe 5 katika kila shule. Wajumbe hawa ni mwalimu mkuu; mjumbe mmoja wa kamati ya afya shuleni (ndiye atakuwa mkuu wa Kamati ya ‘Elimu-Jumuishi’ shuleni); walimu 2 wachapakazi; na mwana-ustawi wa jamii wa shule.</p> <p>Watachukua mafunzo kuhusu sera na kanuni za ‘elimu-jumuishi’ shuleni (kwa masaa takriban 36). Mkuu wa kamati ndiye kiunganishi baina ya shule na kurugenzi ya elimu.</p>


Elimu-jumuishi: vikwazo na ufumbuzi wake Zanzibar



Vikwazo	Ufumbuzi(halisi au mapendekezo)
<p>Uhaba wa zana/vifaa ya kufundishia na kujifunza</p>	<p>Tunaweza kuhamasisha wananchi kuchangia shule. Kuna vitu vilivyo nyumbani ambavyo hutupwa lakini watoto wanaweza kuvileta shule.</p> <p>Tunaweza pia kuendesha mafunzo kuhusu kuandaa vifaa kienyeji na kupata walimu kuchangia mawazo.</p> <p>Tunashawishi serikali kutoa pesa kwa ajili ya 'elimu-jumuishi' na kwa vifaa ambavyo hatuwezi kuitengeneza wenyewe.</p> <p>Watoto wanaweza pia kutengeneza vifaa kamavile jedwali za alfabeti/abjadi na picha mbalimbali zinazoweza kuwekwa madarasani badala ya walimu kununua. Hii ni njia mojawapo ya kuwashirikisha wanafunzi pia.</p>

<p>Mwelekeo hasi wa wazazi kuhusu elimu kwa watoto walemavu.</p>	<p>Tunatumia maigizo na watu kutoka mashirika ya watu walemavu kuongea na wazazi ili kusaidia kuwabadilisha mwelekeo.</p> <p>Pia tunatumia redio na televisheni kutoa ujumbe kuhusu haki na uwezo wa watoto walemavu.</p> <p>Wazazi wanaanza kuona kuwa hakuna kisichowezezana kwa watoto hawa.</p>
<p>Kutofikika kwa mazingira</p>	<p>Hatuzingatii kuzifanya shule zifikike tu, bali kusaidia na kushauri namna ya kufanya sehemu zingine zifikike ili watoto wengi katika jamii (walemavu) waweza kuingizwa shule.</p> <p>Katika uchunguzi wetu wa awali tulichunguza maeneo ya wanajamii kama yanafikika.</p> <p>Tulikwenda vijijini na kuongea na wazazi kuhusu kuyafanya maeneo yao yafikike kwa urahisi kwa watoto walemavu na wazee. Kaya/familia mbalimbali zilihamasishwa kujenga na kuziba mitaro, n.k.</p>
<p>Ukosefu wa utaalam miongoni mwa walimu.</p>	<p>Kwa sasa katika vyuo vya ualimu kumeingizwa vipengele vya 'elimu maalum' na 'elimu-jumuishi' katika programu ya mafunzo ya walimu kazini ili kuhakikisha walimu wanapata stadi na ujuzi wa kufundisha watoto wenye mahitaji maalum (walemavu). Tunayo miongozo mingi na ya kutosha kwa walimu.</p> <p>Wamekuwa na mafunzo ya kina juu ya kuandaa, kufundisha masomo, n.k. Yote haya yanatusaidia kukwepa kuwaacha watoto katika darasa moja kwa muda wote mpaka wanafanya mitihani. Wakihama madarasa wanakwenda na taarifa yao ya maendeleo; na mwisho kabisa wanakuwa wamepata stadi za maisha za kutosha.</p> <p>Idara ya Ukaguzi imehusishwa na mafunzo haya kwa sababu wao husimamia na kutoa ushauri kuhusu mchakato mzima wa kufundisha na kujifunza mashuleni. Kabla ya 'elimu-jumuishi' kuanzishwa mashuleni, walimu walidai kwamba wakaguzi hawakuwa wakieleza chochote kuhusu watoto walemavu - hii ni kwa sababu hawakujua chochote. Kwa sasa wamefunzwa na wanajua nini cha kukagua kwa watoto hawa.</p>

Elimu-jumuishi: vikwazo na ufumbuzi wake Malawi⁵



Vikwazo	Ufumbuzi (halisi au mapendekezo)
<p>Kutokuwepo kwa sheria, sheria za Bunge na sera nzuri kuhusu 'elimu-jumuishi' kunafanya utekelezaji mzima uwe mgumu.</p>	<p>'Elimu-jumuishi' nchini Malawi ndiyo inatangazwa na serikali imeonekana kuvutiwa nayo. Idara ya Elimu Maalum inatakiwa kumaliza muswada wa sera, na Bunge nalo linatakiwa kuupitisha muswada huo na kuifanya 'elimu-jumuishi' kuwa sheria.</p> <p>Tunatakiwa kushirikiana na wananchi wa kawaida ili waelewe umuhimu/faida za elimu-jumuishi na waweze kuwashawishi wabunge wao kulivalia njuga suala hili bungeni.</p> <p>Tunatakiwa kutumia jumuiya mbalimbali zenye wito wa 'elimu-jumuishi' na kuhamasisha vyombo kuwahamasisha wanasiasa na wapanga-sera kuweka sera nzuri kuhusu 'elimu-jumuishi' policies.</p>

⁵ Kwa bahati mbaya nukuu (notes) za majadiliano kuhusu kielelezo hiki hazikuchukuliwa za kutosha.

Serikali ya Malawi imechukua hatua zifuatazo kuendeleza 'elimu-jumuishi':

- kusaini maazimio na mikataba mbalimbali kuhusu haki ya elimu kwa watoto wote
- kuanzisha idara ya elimu maalum katika wizara ya Elimu
- kuhamasisha makao makuu kushirikiana na idara nyingine wizarani
- kupitia mitaala na kuingiza masuala ya 'elimu maalum' kama vipengele muhimu
- kuanzisha kitengo cha elimu maalum katika vyuo vya kawaida vya ualimu na vyuo vikuu
- kuanzisha sera ya elimu maalum na elimu-jumuishi
- kuongeza bajeti ya kitengo cha elimu maalum
- kuongeza hamasa kuhusu ujumuishi wa watu walemavu katika elimu kwa kutumia jumuiya za vyama vya wanajamii, wachapishaji, matangazo kwenye mtandao, mabango na vipeperushi
- kufanya kampeni za kuongeza hamasa kwa wadau wote wa elimu (mf. viongozi wa elimu, walimu, na wanajamii)
- kushirikiana kati ya mashirika ya maendeleo na miradi ya 'elimu-jumuishi'
- kukarabati vifaa mbalimbali na kuvifanya vipatikane kirahisi.

Shirika la kimataifa linaloshughulikia watu wenye matatizo ya macho ndilo linaendesha mradi wa 'elimu-jumuishi' nchini Malawi-(MIEP). Shirika hilo linawawezesha watoto walemavu (hususan wale wenye upofu/matatizo ya macho) kwenda kusoma katika shule za kawaida, karibu na majumbani kwao, na hivyo kuwawezesha kuendelea kuishi nyumbani na familia zao. Hii inawasaidia watoto hawa kuendelea vizuri. Wanafunzi hawa hufundishwa na mwalimu wa kawaida darasani ambaye hupewa ushauri na mwalimu mwenye taaluma ya elimu maalum anayepitia shule mbalimbali kusikiliza na kutoa ushauri unaohitajika. Shirika hili la MIEP linashughulikia Elimu katika wilaya 12 kati ya 34 nchini Malawi.

Serikali ya Malawi hutoa mafunzo kwa walimu wa elimu maalum, mishahara yao na marupurupu mengine, na vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunza. Shirika hilo limetumia mbinu zifuatazo kuifanya elimu nchini iwe 'jumuishi' zaidi:

- kuboresha ushiriki wa walimu wenye taaluma ya 'elimu-maalum' kwa kuwapatia pikipiki au baiskeli na masurufu kwa ajili ya ukarabati wake
- kutoa vifaa vya kufundishia watoto walemavu (macho)
- kutoa vifaa vya kuona kwa watoto wenye matatizo ya macho
- kutoa pesa kwa operesheni za macho
- kuitangaza 'elimu-jumuishi' kupitia jumuiya mbalimbali za jamii
- kutoa ushirikiano kwa wizara ya elimu kuangalia na kusimamia mradi kikamilifu.

Mikakati yote hii imeongeza idadi ya watoto wasiojiweza kujiandikisha mashuleni. Shule nyingi zinawajumuisha watoto wasioona na waalimu zaidi wa kawaida wanajitokeza kuwafundisha watoto hawa. Changamoto imebakia ni namna gani ya kuleta 'ujumuishi katika elimu' katika wilaya 22 zilizobakia.

Vikwazo na ufumbuzi – wakati wa ziara mashuleni

Kama sehemu ya mchakato mzima wa Warsha, washiriki walipangwa katika vikundi vidogo vidogo na kila kikundi kilifanya ziara katika shule mojawapo ya shule 7 zenye 'elimu-jumuishi' Zanzibar. Vikundi vilipangwa na mwendeshaji wa warsha kwa kuzingatia mchanganyiko wa watu na kazi zao, na nchi walikotoka na kuhakikisha kila kikundi kina wazungumzaji wa kutosha wa Kiswahili ili kurahisisha tafsiri pale inapolitajika.



Wanasemina walikuwa wameelezwa kwa kifupi kuhusu ziara mashuleni ili kuhakikisha kuwa wanajifunza na kunufaika kutokana na zaira hizo. Walioneshwa njia kadhaa za kuwasaidia kuona, kuchunguza, kurekodi na kushirikiana kikamilifu. Kwa mfano, kulikuwa na majadiliano kuhusu jinsi ya kufanya uchunguzi wa madarasani, jinsi ya kujiandaa, nini cha kuangalia, na namnaya kuchukua nukuu baada ya kuona jambo. Wanasemina walielezwa kufanya majadiliano ya kina na wakuu wa shule, walimu, na wanafunzi - wanasemina walielekezwa jinsi ya kufanya yote hayo. Zaidi ya yote, wanasemina waliombwa wautumie muda huo kubadilishana mawazo na uzoefu wao na mashule. Walipata changamoto la kutakiwa kuchangia uzoefu wao, mawazo, au hata ushauri wao shuleni.⁶



Ziara mashuleni ziliwasaidia wanasemina kuona masuala mengi yahasuyo 'elimu-jumuishi'. Walibaini masuala mengi zaidi ya yale waliyokuwa wakijadili kabla ya ziara. Hii ilisaidia sana kwenye mjadala wa siku ya mwisho ya warsha kwani kila mmoja alikuwa na mawanda mapana kuhusu 'elimu-jumuishi'. Kwa mfano, yafuatayo ni masuala 'mapya' yanayoweza kuwa matokeo mazuri au mabaya ya 'ujumuishi katika elimu' ambayo yalibainika wakati wa ziara mashuleni:

⁶ Maelezo zaidi ya njia za ziara mashuleni yapo kwenye vipoti ndogo. Ripoti ndogo ya nyongeza inayoonesha taarifa za vikundi za kina imetayarishwa ili iwe marejeo kwa shule zilizotembelewa.

- idadi ya zana za kufundishia zilizooneshwa madarasani
- hali ya jumla ya shule (kama ni nzuri au la, na kama mwalimu mkuu alishirikishwa)
- wavulana kuacha shule na kwenda kufanya kazi
- watoto kupata na njaa au kiu shuleni
- kiwango cha mawasiliano/kuchanganyika baina ya wavulana na wasichana
- lugha ya kufundishia (kama ni lugha-mama au lugha ya pili/nje)
- maudhui ya somo/mtaala
- idadi ya walimu wa kike na wa kiume, na hasa walimu wa kike mashuleni (na athari yake kwa wanafunzi wavulana shuleni)
- masuala mengine ya mazingira zaidi ya yale ya wazi kama ngazi, vyoo, n.k. - pamoja na suala la usumbufu wa kelele kutokana na kukosekana kwa kuta za kutosha za madarasa
- utunzaji wa rekodi/kumbukumbu, mipango ya elimu na mazoezi/majaribio kwa wanafunzi, na utoaji au usambazaji wa habari kuhusu 'elimu-jumuishi'.
- dini (kama dini zote zimepewa nafasi shuleni)
- njia za kufundishia (kama zilimshirikisha mtoto –au zilikuwa za mihadhara tu ya walimu).

Wanasemina walieleza wazi yote waliyoyaona na kusikia mashuleni. Ufupisho wa aina kuu za vikwazo na ufumbuzi wake umeoneshwa hapo chini. Hata hivyo kuna baadhi ya vikwazo ambavyo bado havijapata ufumbuzi wake, ama shule/wageni hawakupata ufumbuzi wake; ama ni vikwazo ambavyo havikujadiliwa kubisa kutokana na ufinyu wa munda. Msomaji angependa kuona kama wanaweza kufikiria mawazo yao kuhusu ufumbuzi wa vikwazo hivyo.

Vikwazo (vilivyo patikana katika shule zaidi ya moja)	Ufumbuzi uliojaribiwa au unaotarajiwa kufanywa na shule
<i>Vikwazo ya kimazingira</i>	
Kukosekana kwa nafasi madarasani/viwanja vya shule	Wangependa kujenga madarasa zaidi (shule ya Mwanakwerekwe F)
Kutofikika kwa vyoo, na hata uhaba wake kwa wavulana ha wasichana	Mipango inaendelea kuvikarabati ili vifikike kwa watoto wote. (shule ya Kusini)
Baadhi ya mazingira hayafikiki, mf. Njia za miamba, ngazi, njia za walemavu, mitelemko mikali, n.k.	Kamati ya shule imeshaanza mipango ya kujenga vyoo, n.k. (shule ya Mwanakwerekwe Imeshaanza kuboresha mazingira ya shule (shule ya Mwembe Makumbi) Njia za baiskeli za kusumwa/walemavu kuelekea ofisi ya mwalimu mkuu na baadhi ya madarasa zimeanza kujengwa. (shule ya Paje)
Uhaba wa maji yaliyopo shuleni.	

Mazingira ya kelele kutokana na kuta chache zinazotenga madarasa – siyo bora kwa kujifunzia	
Ukosefu wa viwanja vya michenzo	
Umbali mrefu wa kwenda shuleni	
Vikwazo vya kimwelekeo	
Mwelekeo hasi wa jamii na baadhi ya wazazi kuhusu 'elimu-jumuishi' (na hususan wale ambao wana watoto katika vitengo/madarasa maalum)	<p>Mipango imeshafanywa ya kuwahamasisha wazazi (shule ya mwanakwerekwe F)</p> <p>Kamati za wazazi na walimu zinaendelea kuelimisha jamii kuhusu elimu-jumuishi (shule ya Kusini)</p> <p>Kuna vikao na mikutano inayojadili masuala ya ulemavu na 'elimu-jumuishi' (shule ya Mwembe Makumbi)</p> <p>Jamii kwa sasa inashirikishwa katika kuitekeleza 'Elimu-jumuishi' (shule ya Paje)</p>
Mwelekeo hasi wa walimu (kipindicha nyuma)	<p>Kwa sasa kuna walimu waliohamasika na elimu-jumuishi na wanajitoa kikamilifu (shule mwana kwerekwe F)</p> <p>Kwa sasa walimu wanapendelea kujifunza zaidi kuhusu elimu-maalum na elimu-jumuishi (shule ya mwanakwerekwe E)</p>
Mimba miongoni mwa wasichana (mwelekeo hasi wa shule na jamii kuhusu hali hiyo)	
Urahisi wa kupata kazi unawafanya wavulana kuacha shule	
Vikwazo Vya Ki Utendaji	
Njia za kufundishia (hazivutii ujumuishi)	Mafundisho ya ziada kwa watoto wanaopata chini ya wastani hutolewa kila Jumamosi na Jumapili (shule ya Mwanakwerekwe E)
Watoto walemavu wanalazimishwa kubakia madarasani mwao	
Walimu wanaonekana kufikiria vikwazo vya kimazingira tu	Kwa sasa wanafunzi wengi wanachunguzwa mahitaji na uwezo wao (shule ya mwembe makumbi)
Utofauti wa 'maazimio' ya ufundishaji yaliyopo yanatumia muda mwingi kwa watoto walemavu na wasio walemavu	Serikali inapaswa kubadili muhtasari ili uweze kuondoa utofauti huo (shule ya Jangombe)

Kuwepo kwa vitengo au madarasa tofauti kwa elimu maalum	
Dini moja tu kufundishwa shuleni, je watoto wa dini zingine wanatengwa?	
Wavulana na wasichana wanatenganishwa	
Vikwazo vya miundo - mbinu	
Ufinyu wa bajeti ya shule	Kuomba pesa zaidi serikalini (shule ya Mwanakwerekwe) Wangependa kupata pesa zaidi kusaidia utekelezaji wa 'elimu-jumuishi' (shule ya Mwembe Makumbi)
Uhaba wa vifaa vya kufundishia/kujifunza, na vifaa-saidizi, samani, n.k.	Plans exist for obtaining teaching materials [Mwanakwerekwe E school] Teaching/learning materials are present [Paje school] More meetings with parents and community in general to discuss solutions to the problem of inadequate furniture [Jang'ombe school]
Uchache wa walimu wenye sifa na walimu wenye ujuzi/stadi za kusaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum/walemavu au hata watoto wote	Kumeanzishwa mafunzo bora kwa waliku – hufanywa shuleni na katika lugha-mama (shule ya kusini) Mafunzo yanaendelea kutolewa kwa walimu (shule ya Mwembe Makumbi)
Hakuna vifaa vya kutosha kutumia Breili, au kufasiri lugha ya ishara	
Hakuna mafunzo ya kutosha kuhusu masuala ya ulemavu	
Wingi wa watoto darasani	
Mishahara midogo ya walimu	

4. Hatua zinazofuata

4.1. Kubainisha vikwazo maalum na ufumbuzi wake

Kwa muda wote wa warsha, wanasemina walianza kufikiria kwa makini zaidi kuhusu vikwazo vya 'ujumuishi' katika elimu na ufumbuzi wake. Wanasemina walikumbushwa kahusu tofauti zilizopo kati ya vikwazo vya jumla na ufumbuzi wake, na vikwazo mahsusi na ufumbuzi wake:

Mfano wa kikwazo cha jumla: ufundishaji mbovu/mbaya.

Mfano wa kikwazo mahsusi: walimu kutumia njia mbaya kufundisha kama vile kusimama mbele ya darasa na kuwasomea kitabu bila kuwashirikisha wanafunzi.

Mfano wa ufumbuzi wa jumla: kuwahamasisha walimu

Mfano wa ufumbuzi mahsusi: kushirikiana na mkufunzi wa chuo cha mafunzo ili kuanzisha programu ya mafunzo ya walimu-kazini ambayo yatawahamasisha na kuwawezesha walimu kutumia njia-shirikishi za kufundishia.

Kadri tunavyokibainisha kikwazo mahsusi, ndivyo inavyokuwa rahisi pia kufikiria ufumbuzi wake mahsusi. Na tukibainisha ufumbuzi mahsusi inakuwa rahisi pia kupanga namna sahihi ya kutatua kikwazo husika. Ni vigumu kuweza kupanga orodha au namna sahihi ya kufumbua tatizo kwa ufumbuzi wa jumla kama 'kuwahamasisha walimu'. Lakini kama tukiangalia ufumbuzi mahsusi wa hapo juu, inaweza kuwa rahisi kwetu kufikiria namna /orodha ya shughuli zitakazotusaidia kupata ufumbuzi. Kwa mfano:

- kuonana na mkuu wa chuo cha ualimu
- kusoma makala mbalimbali kuona jinsi nchi nyingine zinavyoendesha programu hiyo
- kuwashirikisha walimu kujua mafunzo gani wangependa kupata – kutumia masaili na majadiliano ya vikundi
- kuwashirikisha wanafunzi kujua wangependa walimu wao wawe namna gani – kutumia michezo ya kuigiza na picha kuwasaidia kutoa mawazo au maoni yao
- andika/andaa programu ya mafunzo kwa nguvu mpya, ifanyie majaribio katika shule tano na itathmini baada ya kipindi cha miezi sita.

Kwa hiyo swali linalofuata ni kwamba: ni namna gani tunaweza kubainisha kwa ukamilifu zaidi vikwazo 'mahsusi' na ufumbuzi wake kuhusu 'elimu-jumuishi' katika sehemu zetu? Baadhi ya wanasemina waliona ni vigumu kufikiria vikwazo mahsusi na utatuzi wake. Hii inawezekana ni kwa sababu hawakuwa na data za kutosha walipokuwa mbali na mazingira yao ya kazini. Muhimu ni kuwa watakaporudi makwao wanasemina wote washirikiane na wenzao na wadau wengine kukusanya habari zaidi ili waweze kubainisha vikwazo mahsusi na ufumbuzi wake.

4.2. Kutumia utafiti-kwa-vitendo

Mchakato wa 'tazama – tafakari – tenda' (utafiti-kwa-vitendo) utatusaidia kufanya uchunguzi mahsusi zaidi wa matatizo/vikwazo; kuchambua habari /data na kufikiria ufumbuzi; na kisha kuchukua hatua sahihi kwa vitendo ili kupata ufumbuzi.

Mawazo yafuatayo yalitolewa kwa wanasemina kama vitendo ambavyo vingewasaidia katika mchakato wa 'tazama – tafakari – tenda'. Alama ya vema(✓) inaonesha matendo yaliyotendwa wakati wa warsha.

Tazama

- Tafuta kadri uwezavyo matatizo au vikwazo, na ni nini kilichokwisha fanyika kuvitatua vikwazo hivyo
- Ongea na watu wa aina zote, kwa kutumia mfano:
 - chemshabongo (✓)
 - majadiliano ya vikundi (✓)
 - kusimulia hadithi (✓)
 - masaili (✓)
- Chunguza na kurekodi kwa kutumia mfano:
 - uchunguzi darasani (✓)
 - picha (✓)
 - video (✓)

Tafakari

- Wewe, wenzako na wadau – mnachambua yote mliyosikia, kuona, na kurekodi.
- Tumia njia mbalimbali kusaidia watu kuchambua data na kuzitafakari kwa kina.
- Tumia vielelezo anuwai, kama vile:
 - vielelezo vya mlima (✓)
 - mstari wa wakati
 - ramani
 - vikaragosi/vikatuni/michoro (✓)
- Tumia matendo, kama vile:
 - drama/tamthiliya
 - maigizo (✓)
 - maonesho ya vibaraka
 - kucheza/kuimba
- Tumia mazoezi ya kuandika na kusoma, kama vile:
 - kumbukumbu (rejea) za kila siku
 - majaribio ya utafiti/yaliyotafitiwa
 - hadithi na makala kuhusu mawazo na uzoefu binafsi (✓)

Tenda

- Fanya majaribio.
- Jaribu kufanyia kazi mawazo ambayo:
 - unayo kuhusu kuboresha mazingira/hali
 - wenzako wameshayatumia
 - uliyasoma katika jarida la EENET
 - mwanafunzi au mzazi kayapendekeza.

- Njia ya utafiti-kwa-vitendo katika kupanga kazi itakujulisha kuwa hakuna ufumbuzi maalum ambao utafaa kila sehemu.
- Unajaribu mambo – kama yanafaa unayaboresha mengine zaidi na kisha unayaribu.
- Kama hayafai – unafikiria mengine zaidi, na kuyajaribu.

Mpango binafsi

Wanasemina walielezwa kufikiria namna ambavyo wanaweza kutumia mchakato wa ‘tazama – tafakari – tenda’ katika ‘elimu-jumuishi’ watakaporejea nchini kwao. Walielezwa kufikiria maswali yafuatayo. Walijadiliana, lakini walitakiwa pia kuandika mpango binafsi.

- Ni matendo/mazoezi gani utakayofanya kukusaidia kuchunguza kwa makini vikwazo mahsusi na ufumbuzi wake katika mazingira yako?
- Ni matendo/mazoezi gani utakayofanya kukusaidia kuchambua data na kufikiria/kupata ufumbuzi mahsusi wa vikwazo?
- Ni wepi utafanya nao matendo/mazoezi hayo?

Mifano ifuatayo ilitolewa na washiriki wa warsha:

“Mpango wangu – mfano wa baadhi ya matendo mahsusi ya kunisaidia ‘kutazama – kutafakari – kutenda”.

Tazama

Nitatumia picha na watoto kutoka shule tatu za wilaya yangu kuwasaidia kunieleza wanapenda/hawa pendi nini katika shule zao. Kisha nitatumia njia ya masimulizi na walimu wao.

Tafakari

Nitatumia vielelezo vya mlima na ramani wakati wa mkutano na maafisa elimu ili vitusaidie kuchambua data tulizokusanya, na kufikiria/kuweka mapendekezo ya ufumbuzi wa vikwazo.

Tenda

Tutafanya jaribio kwa kutumia kitendo/vitendo sahihi kwa kuzingatia data tulizokusanya na mawazo yetu ya pamoja.

Kisha

Tutachunguza tena baada ya miezi michache kuona kama jaribio letu limefanikiwa.

Tutashirikiana na watu wengi zaidi ili kuboresha zaidi.

Tutafanya mazoezi/majaribio zaidi na zaidi.

Tutaendelea kuboresha elimu!

Majibu ya wanasemina

Wanasemina walitumia muda kadhaa kuhusu mipango yao ingawa jaribio/mazoezi hayakutoa matokeo waliyoyatarajia. Matatizo ya jumla mawili yalionekana; nayo ni kutaka kutumia mpango uliozoeleka katika shule husika badala ya mpango binafsi, na kutoelewa jinsi ya kushirikiana na wadau kwa misingi ya usawa katika masuala haya ya majaribio.

Mawazo mbalimbali kuhusu kupanga

Wanasemina wengi walianza kuweka mipango ya projekti (malengo, madhumuni, viashiria, n.k). mipango hiyo ilieleza kwa mapana vipengele vya projekti ya ‘elimu-jumuishi’ badala ya kutumia mipango rahisi kama vile kutoa kauli binafsi ya kudhamiria kufanya matendo-shirikishi na wenzake na wadau pia. Hii ni kwa kuwa tumezoea kupanga mipango kwa nia ya kuwavutia wafadhili, kitu ambacho hatupendi kujadili au kuandika mipango yetu binafsi. Muda zaidi unahitajika (kuliko ule uliokuwa ukitumika) ili kuwawezesha washiriki kufikiri na kutenda/kutumia mbinu za mkabala ‘mpya’ kama ule wa ‘utafiti-kwa-vitendo’.

Je, kushiriki kwa mdau kuna maana gani?

Baadhi ya wanasemina walitatizwa na jinsi ya kuwashirikisha wadau katika mchakato wa ‘tazama – tafakari – tenda’. Wakati wa kujadi swali la “nani utashirikiana nao katika utekelezaji” baadhi ya wanasemina walitoa orodha ndefu. Orodha hii haikuwa inaaksi au kuashiria kikamilifu makundi ya watu ambao wangestahili kufanya au kuwa na uzoefu wowote katika elimu na jamii. Baadhi ya wanasemina waliorodhesha vikwazo au matatizo ambayo wangewauliza wadau katika vikundi, n.k. Hata hivyo ni bora zaidi kumshirikisha mdau katika kutaja/kueleza vikwazo anavyofahamu, vikwazo anavyoviona kama muhimu zaidi, na ufumbuzi wake ambao anauona kama ndiyo unafaa (au waliwahi kusikia ulifaa sehemu zingine). Tukiwaeleza wadau vikwazo, tutakuwa tunawanyima nafasi ya kutueleza mambo mapya ambayo hatukuwa nayo kabla au hatukuyafikiria au kuyasikia kabla. Lazima tuchukue hadhari kwa hili.

5. Ufupisho wa masomo na mapendekezo

Kuna taarifa nyingi katika kazi zilizokuwa zinawasilishwa na wanasemina kuhusu ‘elimu-jumuishi’; na pia kutokana na majadiliano ya vikundi; mazoezi anuwai ya warsha, na vile vile kutoka tathmini ya warsha. Ufupisho wa masomo/vipindi /mawazo muhimu umewasilishwa hapa chini kama ifuatavyo:

Sera na mipango

Kuhamasisha mchakato wa mabadiliko ya sera

- Sera ambayo inasaidia ujumuishi ni muhimu. Hata hivyo hatuwezi kusubiri serikali kufanya mabadiliko ya sera kabla sisi wenyewe hatujaanza kufanya mabadiliko katika elimu. Tunapaswa kuongoza mabadiliko ya sera kwa kuwa kielelezo bora cha mabadiliko hayo.
- Ili kusaidia katika mabadiliko ya sera, tunapaswa kuwa na uelewa wa mambo mengi kiasi kwamba tunaweza kutoa hoja zenye mashiko wakati tunapotangaza na kushawishi. Hivyo tunatakiwa kupeana taarifa za kimataifa ili kujifunza mafanikio na matatizo ya michakato ya kubadili sera kutoka nchi mbalimbali.
- Itasaidia pia tukianzisha shule za majaribio ambazo zitaonesha “elimu-jumuishi kwa vitendo”. Shule hizo zinaweza kusaidia viongozi (wapanga sera) wa serikali kuona tunachomaanisha kwa ‘elimu-jumuishi’ na pia kutumika kama maeneo ya kujaribia njia mpya ambazo zitaweza kusambazwa na kutumika katika shule zingine.

Sera na mipango thabiti

- Sera za elimu-jumuishi zinapaswa kuwa jumuiishi hasa, ambazo siyo tu kwa masuala ya ulemavu, bali pia kwa masuala ya haki za wasichana wanaokatiywa shule kwa sababu ya mimba, na umuhimu wa kutumia lugha ya nyumbani (lugha-mama) kufundishia (hususan kwa miaka ya mwanzo ya masomo).
- Masomo ya msingi mzuri yanahitajika (kabla ya kuanza sera na mipango mipya) ili kuonesha yaliyopo na yanayohitajika. Hata kama hatukuwa na msingi mzuri wa masomo wakati tunaanzisha projekti yetu, bado tunaweza kufanya sasa ili kuweza kulinganisha na wakati ujao.
- Kila sehemu itahitaji kuwa na mpango wake tofauti (mahsus), ili kushughulikia vikwazo vyake, rasilimali zake, wadau waliopo, na kadhalika. Tunatakiwa wote kufikiria ufumbuzi kufuatana na s ehemu zetu – ingawa tuna weza kupata mawazo kutoka nje, lakini hao hawawezi kutupa ufumbuzi wa matatizo yote.
- Idara za ‘elimu maalum’ katika wizara za elimu zinaweza kutusaidia kupanua elimu-jumuishi. Hata hivyo tunapaswa kuwa makini nazo ili kuwepo kwake kusizifanye idara zingine za elimu kupuuza “ujumuishi” na kudhani kuwa elimu-jumuishi ni kazi ya mtu au watu fulani.

Mazoezi ya darasani/ufundishaji na mitaala

Mwelekeo, Tabia na Matendo:

- Elimu-jumuishi inatutaka tuwe na njia za ufundishaji (na mitaala) ambazo zitawezesha ujumuishi wa watoto wote katika ngazi za “kuwepo, kushiriki, na kunufaika (kupata maarifa).
- Tunatakiwa tuboreshe namna ya kupanga elimu na rekodi ya mwanafunzi mmoja mmoja, na hasa kwa kuwa na njia sahihi za kutahini mitihani kwa watoto wote.
- Nafasi ya maigizo katika elimu lazima izingatiwe sana – kwani inaweza kuonesha bayana kama watoto wanajisikia kujumuishwa na kufurahia shuleni, na huweza kuathiri mahudhurio yao na hata kushiriki kwao shuleni.
- Namna dini zilivyoingizwa katika mtaala wa elimu na ufundishaji lazima izingatiwe pia – hii ni kwa sababu asili na namna ya mafundisho ya dini mbalimbali yanaweza kuwatenga baadhi ya watoto.
- Kazi za vikundi zinaweza kuwa njia thabiti katika ufundishaji na kujifunza hata wanafunzi wakiwa wengi kiasi gani. Wanafunzi ni muhimu kushirikishwa katika kugawa na kuongoza vikundi vyao.
- Tunaweza kuhawilisha kule madarasani aina ya mazoezi shirikishi tunayofanya katika warsha/semina, ili kuyafanya yawe hai na ya kumlenga mtoto kwa kusisitiza ufumbuzi wa matatizo na kujenga stadi anuwai za mtoto.

Vifaa:

- Tunatakiwa kuwa wabunifu wa kutengeneza na kuandaa zana mbalimbali za kufundishia na kujifunza. Tusiruhusu ukosefu wa pesa kuwa kikwazo kikubwa sana, na bado tunaweza kuwashirikisha hata wanafunzi kutengeneza vifaa asilia na rahisi (kwa mf. kutengeneza zana kwa kutumia vitu vilivyotupwa majumbani, kuwaeleza watoto watengeneze zana na kuzionesha shuleni, n,k,).
- Watoto wanaweza kwenda shuleni na kujifunza vizuri hata kama hatuna zana maalum, za kisasa. Badala ya kusubiri pesa za kuagizia vifaa au mafunzo, tunapaswa kujitahidi zaidi kutafuta njia nyepesi, za asili, na za kudumu za kutengeneza vifaa na stadi (kama vile kuwaalika wenyeji wazee na mashirika ya walemavu kusaidia walimu/wanafunzi/wazazi kujifunza na kutumia ligha ya ishara, breili, n.k.).

Kozi na mafunzo ya ualimu

Wepi tuwape kozi na mafunzo?

- Namna tunavyoteua walimu walio kazini kwa ajili ya mafunzo zaidi ya elimu-jumuishi inabidi tuboreshe, ili tusijikute tunatoa mafunzo hayo kwa wale tu walio tayari na imani katika ujumuishi.
- Maafisa-elimu ukaguzi na watahini pia wanatakiwa kujielimisha ili waweze kuwasaidia walimu katika mwelekeo mpya wa ujumuishi, na pia kuhakikisha kuwa walimu wanatumia njia mpya walizojifunza.
- Watumishi wa shuleni wasio-walimu pia wanapaswa kufahamu na kusaidia misingi ya ujumuishi hata kama hawafundishi moja kwa moja madarasani au kushiriki uongozi wa shule.
- Ni muhimu kuelewa nafasi ya walimu wakuu mashuleni. Bila ya msaada wao ujumuishi hauwezekani mashuleni. Tunataka walimu wakuu wenye kufahamu

ujumuishi, na walio tayari kuhamasisha wafanyakazi wote shuleni kuhusiana na elimu-jumuishi.

- Usawa kati ya walimu wa kike na wa kiume ni muhimu katika viwango vyote ili wasichana na wavulana waweze kusaidiwa wakati wote wawapo shuleni. Hii itasaidia kuzuia wanafunzi kuacha shule.
- Watu walemavu wahamasishwe na kusaidiwa kujifunza kuwa walimu ili waweze kuwa kielelezo sadifu kwa wanafunzi walemavu na kupata haki sawa ya kuajiriwa kama walimu.
- Walimu wote wanapaswa kuelimishwa tangu mwanzo wa mafunzo yao njia za kufundishia/kujifunza zinazomshirikisha mtoto kwa sababu njia hizo huboresha kujifunza kwa mtoto. Kujifunza njia hizi kusiwe tu kwa walimu wa 'elimu maalum' bali pia kwa walimu wote.

Ni yepi yaliyomo katika Mafunzo?

- Mafunzo hayamaanishi tu kozi rasmi kuhusu elimu-jumuishi. Walimu wanaweza kujifunza mengi kuhusu ujumuishi zaidi kwa kujadiliana miongoni mwao, na kwa kuyafanyia kazi mawazo mapya mashuleni.
- Tunatakiwa kutafuta njia za kuwamotoisha na kuwahamasisha walimu katika kazi yao hata pale wanapokabiliwa na changamoto na mageuzi ili waweze kuendelea na kazi badala ya kutoroka toroka, n.k.
- Mafunzo ya elimu-jumuishi kwa walimu yanapaswa kuendelea kutolewa katika lugha ya taifa ili kuboresha ufahamu wao na umilisi wao wa njia mpya za kufundishia na kujifunza. Hii inamaanisha kuwa wafadhili wanapaswa kugharimia pesa zaidi katika kutafsiri vifaa na vitabu vya kusoma vya mafunzo katika Lugha ya Taifa.
- Walimu hawapaswi kufundishwa tu kuhusu elimu-jumuishi, bali wanahitaji pia kujua haki za mtoto/binadamu na masuala ya ubaguzi, kutengwa, n.k.

Ushirikishwaji wa Wadau

NGOs/DPOs

- Mashirika yasiyo ya serikali (NGOs) yote yanayoshughulikia elimu yashirikiane kwa karibu zaidi, yajadili ujumuisho na yahakikishe tunafanya kazi kwa lengo moja, na siyo kupingana.
- Kunapaswa kuwa na ushirikiano imara na programu za 'CBR' – elimu -jumuishi na CBR zinapaswa kushikamana.
- Matumizi makubwa ya mifano na vielelezo kutoka kwenye 'DPOs' na jamii nzima yanaweza kusaidia kazi yetu ya kuwahamasisha na kubadili mwelekeo wa jamii kuhusu ujumuishi.

Jamii na Wazazi

- Tunapaswa kuwashirikisha watu muhimu na viongozi wa kidini katika jamii ili waweze kufikisha ujumbe wa elimu tunaowapa wazazi (mara nyingi watu hawa wana nguvu ya kusikilizwa na wazazi katika jamii kuliko sisi).
- Kuvisaidia vikundi vya misaada vya wazazi ni muhimu pia. Kwa kufanya hivyo, watasaidia kutangaza na kufuatilia ujumuishi katika elimu kwa watoto wao.
- Tunapaswa kuhakikisha kwamba hatuwalaumu wazazi pale watoto wao wanapoacha shule au wasipojifunza kitu shuleni. Pia tusiwafikirie kuwa wazazi wote hawajui chochote kuhusu masuala ya elimu na ujumuishi. Tunapaswa kuwa karkibu na familia zao, kuchunguza sababu za mahudhurio mabaya au

uwezo mdogo wa masomo, na kushiri kiana na wazazi wao kutafuta ufumbuzi kwa pamoja na kwa usawa.

- Kamati za wazazi, wanafunzi, walimu na hata wanajamii zisaidie kuchunguza matatizo ya kuwatenga watoto, kuyatafutia ufumbuzi, na kutoa ushirikiano katika kueneza ujumbe wa ‘ujumuishi’ kwa watu wengi zaidi.
- Matendo ya ubunifu wa hali ya juu yanahitajika ili kutusaidia kuwahamasisha wanajamii na kuwafanya waendeleo kusikliza ujumbe wetu wa ujumuishi. Kwa mfano, matumizi ya vipindi vya redio na tamthiliya yanaweza kusaidia kuwahamasisha watu na kuelewa vizuri ujumbe na hivyo kuenea na kuwafikia watu wengi zaidi.
- Istilahi “uhamasishaji” inapaswa kuepukwa pale tunapokuwa tunadhamiria kupanua welewa wa watu! Istilahi hiyo imekuwa ikitumika vibaya na haina maana moja. Inaweza kutumiwa kirahisi kuficha udhaifu wetu pale tunaposhindwa kujua kazi tunayokuwa tunafanya.
- Watoto na vijana wanaweza kuchangia sana katika kuendeleza ujumuishi na haki zake. Tunaweza kutumia uzoefu wa kazi za watoto, na kuwashirikisha katika mazoezi ya kuchekesha, ili watusaidie namna ya kuwahamasisha watoto kujieleza na kutoa maoni yao kuhusu ujumuishi katika familia zao na jamii kwa jumla.

Kufikika/upatikanaji

- Baadhi ya matatizo ya kimaumbile na kimazingira (na hata ya kisiasa) ambayo huwaathiri watoto kwa kutoshiriki katika elimu huwa yako nje ya uwezo wetu hatuwezi kuyabadilisha. Hivyo badala ya kusubiri matatizo yasiyo na utatuzi, tunapaswa kuwa wabunifu kuyatafutia ufumbuzi. Kwa mfano mfumo wa “kusoma kwa shifti” umesaidia kutatua tatizo la shule zenye idadi kubwa ya wanafunzi wakati uwezo wa kujenga madarasa mapya haupo kwa ukosefu wa pesa.
- Ingawa tunasisitiza na kulenga elimu mashuleni, bado tunapaswa kufikiria kuhusu mazingira yanayoweza kuwa na vikwazo vya kufikika – nayo haya yanaweza kuzuia watoto kufika/kwenda shuleni.
- Tuisahau kuwa “kufikika” hujumuisha masuala mengi zaidi ya majengo kwa wasiojiweza tu. Matalani, shule inaweza kuchukuliwa kuwa haifikiki pale inaposhindwa kutosheleza huduma ya chakula na maji, au kusaidia watoto wanaoshindwa kuleta vitu hivyo shuleni. Shule zisizo na kuta zinazostahili (ambazo hazizuii kelele kati ya darasa na darasa) pia nazo huwekwa katika kundi hilo kwa sababu makelele hugaribu usikivu wa wanafunzi na hivyo kuathiri kushiri na kujifunza kwao. Hali ya shule kwa ujumla pia huweza kuathiri kufikika kwake – kwa mfano kama shule ni rafiki na karimu kwa jamii inayoizunguka, itafikika na kila mtu.
- Misalani ni suala ambalo huathiri ujumuishi katika shule nyingi (hususan unapowauliza watoto maoni yao!). Tunapaswa kuhusisha mambo mengi: idadi ya vyoo, kufikika kwake, mahali vilipo, usalama na usiri, usafi wake, na namna rahisi tunavyowaruhusu watoto kuvitumia.

Shule maalum

- Tunapaswa kuwa wazi kuwa shule maalum na vitengo maalum siyo sawa na elimu-jumuishi.
- Hata hivyo, asasi maalum zinaweza kuchangia sana katika kuendeleza elimu-jumuishi. Tunatakiwa kutafuta namna ya kushirikisha mifumo hii kwa pamoja, ili wataalam wa elimu katika asasi hizi waweze kusaidia walimu wa shule za kawaida – kwa malengo thabiti, ili hatimae kuwa na mfumo mmoja wa elimu unaokidhi mahitaji ya watoto wote.
- Vitengo au shule maalum wakati mwingine vinaweza kutoa hatua ya kwanza muhimu kwa baadhi ya watoto kabla hawajaingizwa katika shule-jumuishi.
- Tusidhanie kuwa katika vitengo au shule maalum zina stadi bora na vifaa kila wakati. Wakati mwingine shule au vitengo hivi hukosa walimu wenye sifa na hata vifaa; na kwa hiyo zinaweza kutoa elimu kwa mtoto mlemavu ambayo iko chini ya yule aliye katika shule-jumuishi (ya kawaida).
- Shule /Vitengo maalum huweza kuendelezwa na kuimarishwa ili hatimae vitumike kama vituo vya mafunzo kwa shule zilizo wilayani humo, au kuwa mahali pa kuwapata walimu mahiri na wataalam wa ujumuishi.

6. Matokeo ya warsha

Matokeo kamili ya warsha au kozi ya mafunzo hayawezi kupimwa mara baada ya tukio. Kwa kawaida watu huchukua muda kuakisi yale waliyosikia, kuona na kujifunza kabla hawajafikiria tena mwelekeo au mawazo yao. Pia inaweza hata kuwachukua muda wa ziada kubadili matendo na sera – kama kweli warsha iliwashawishi au kuwahamasisha kufanya hivyo.

Hata hivyo, matokeo ya awali yanaweza kuonekana kutokana na tathmini ya warsha. Siri Wormnæs, mmoja wa washiriki kutoka Norway, ndiye aliyeongoza mchakato wa tathmini. Kimsingi, washiriki walikuwa wakijibu maswali kila mwishoni mwa siku ya warsha. Wanasemina walikuwa wakiulizwa kuhusu waliyojifunza na yaliyowachanganya kwa siku hiyo. Walikuwa wakiulizwa pia waliyojifunza nje ya warsha (kama vile wakati wa chakula, n.k.). Hatimae waliulizwa namna walivyojisikia kuhusu mabadiliko ya uwezo kutokana na kuhudhuria warsha⁷ hii.

Kufundisha, kujifunza na njia za utafiti

Matokeo yanaonesha kuwa washiriki walifaidi mtindo wa uendeshaji wa warsha wa kuwashirikisha moja moja. Waliiona ni njia nzuri kwani waliweza kubadilishana habari na kukuza moyo wa kujiamini katika kuchangia mazuri na mabaya ya uzoefu wao. Baadhi walieleza katika maoni yao kuwa iliwasaidia kufikiria kwa makini hata misimamo yao ya awali katika baadhi ya mambo. Washiriki walikiri kuwa utafiti uliofanywa, na njia shirikishi zilizotumika kujifunza, (mf. matumizi ya picha, usimuliaji wa hadithi, kazi za vikundi, maigizo, n.k.) vitaweza kutumiwa katika sehemu zao za kazi kuwafundishia walimu au wanafunzi. Walieleza jinsi ambavyo wangeluweza kutumia baadhi ya vitendo na mazoezi katika kazi zao za kila siku na baadhi walionesha dhamira ya kufanya hivyo.

Washiriki wachache waliona baadhi ya mazoezi yalikuwa mageni na ya kuchanganya. Walitoa maoni yao kuwa mazoezi mengi na mapya yalifanywa kwa muda mfupi. Hii inaonesha ugeni wa vitendo au mazoezi kwa baadhi ya wanasemina na umuhimu wa kufanya mageuzi wakati wa kutekeleza njia hizo baadae. Walipoulizwa kutaja mambo matatu waliyojifunza nje ya warsha wakati wa mapumziko, n.k. waliorodhesha mlolongo wa mambo. Waliona kuwa wamejifunza kutoka mfumo wa elimu wa kila mmoja kuhusiana na sera, njia za ufundishaji/kujifunza, tamaduni, serikali na hali za kisiasa, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO's), miundo ya mashule, n.k. Hii inaonesha jinsi kujifunza nje ya mfumo rasmi wa mafunzo au mikutano ilivyo pia muhimu kuzingatiwa.

Kufahamu masuala ya elimu-jumuishi

Washiriki wa warsha walikuja kutoka sehemu na mazingira tofauti, na wote wakiwa na ufahamu na uzoefu tofauti kuhusu elimu-jumuishi kabla ya warsha kufanyika. Wengi wao, warsha iliwasaidia kubainisha dhana ya 'elimu-jumuishi'. Iliwasaidia kuona elimu-jumuishi kama mchakato endelevu ambao hauna tafsiri moja maalum,

⁷ Maelezo kamili kuhusu matokeo ya tathmini yapo kwenye ripoti ndogo.

wala kanuni moja ya ufumbuzi wa matatizo katika maeneo yote. Baadhi waliona ufahamu wao kuhusu elimu-jumuishi umepanuliwa, zaidi ya kufikiria mtizanio wa ulemavu tu. Wengine walijiona kuwa wanaelewa umuhimu wa kugundua na kutatua vikwazo vya ujumuishi zaidi ya vile vilivyo wazi kama vya mazingira, majengo na fedha.

Hata hivyo, baadhi ya washiriki walijiona kama warsha bado iliwaacha njia panda kidogo, kwa kuwa hawakupata fasili halisi ya 'elimu-jumuishi', au njia rahisi na ya mkato ya kutafuta ufumbuzi wa matatizo. Na kwa baadhi, warsha haikuwatosheleza kuweza kutatua au kuzikabili baadhi ya changamoto mahsusi wanazo kabiliwa nazo katika maeneo yao.

Umilisi/uwezo binafsi

Washiriki walitoa majibu mengi kuonesha jinsi uwezo wao binafsi ulivyobadilika kutokana na kuhudhuria warsha hii. Hii ilikuwa ni pamoja na kuboreka kwa uwezo wa kutenda na kujiamini katika kutambua na kuchambua matatizo au vikwazo, na kuyatafutia ufumbuzi kwa njia shirikishi. Baadhi waliona kuwa wangeweza zaidi kuwasilisha masuala na kuyajadili na watu wengine kwa kutumia mbinu mbalimbali za mawasiliano.

Maelezo ya mawasiliano ya washiriki

Name and position	Address	Email address	Telephone and fax
Abualia, Akram Msimamizi wa elimu-jumuishi wizara ya elimu (MOEHE)	MOEHE Directorate of Education Bethlehem and West bank P.O. Box 168 Bethlehem PALESTINE	Akia122@yahoo.com Akia123@hotmail.com	Work: +972 022741271/2 Fax: +972 02-272617 Cell: +972 0522226055
Bakar, Shauri Saleh Mwalimu wa shule ya sekondari Bubwini, Unguja	Ministry of Education and Vocational Training P.O Box 394 ZANZIBAR, TANZANIA		Cell: +255 787041988
Brodtkorb, Svein Mshauri Mwandamizi	Norwegian Association of Disabled P.O. Box 9217 Grønland 0134 Oslo, NORWAY	Svein.brodtkorb@nhf.no	Work: +47 24102480 Cell: +4799624407 Fax: +4724102499
Bruce, Lissen Mkuu wa Idara ya masuala ya Kimataifa	Norwegian Association of Disabled P.O. Box 9217 Grønland 0134 Oslo NORWAY	Lissen.bruce@nhf.no	Work: +47 24102480 Cell: +47 90502102 Fax: +47 24102499
Cortider, Owerodumo Mwalimu Mkuu	Agururu Unit P.O. Box 887 Tororo UGANDA	cortider@yahoo.co.uk	Cell: +256772592190/ +256772556569
Dewan, Pramila Mratibu	P.O. Box 21951, Kathmandu, NEPAL	nnetwork@mail.com.np	Work: +977 14416473 Cell: +977 9841238014

Doya, Yona Gamusi Afisa-elimu wa Wilaya	Tororo District Local Government P.O. Box 490 Tororo UGANDA	rnanima@yahoo.com	Work:+256 772611805/ +256 772627510
Galiwago Kizito, Ahmed Ofisa-elimu wa Wilaya	Kayunga District Local Government P.O. Box 18000, Kayunga UGANDA	agkizito@yahoo.com	Cell: +256772406849 Work (DRO office): +256392762585 Fax: (DRO office):+256392252585
Grimstad, Johan Edvard Mshauri wa Masuala ya Maendeleo	Norwegian Association of Disabled P.O. Box 9217 Grønland 0134 Oslo NORWAY	nhf@nhf.no	Work: +47 24102485 Cell: +47 92266853 Fax: +47 24102499
Hamadi, Hamadi Othman Afisa wa Elimu Maalum	Ministry of Education and Vocational Training P.O. Box 203 Chake Chake Pemba, Zanzibar TANZANIA	spned@zanlink.com	Cell: +255777853944
Handeland, Silje Afisa-programu	NFU P.O. Box 8954 Youngstorget 0028 Oslo NORWAY	Silje.handeland@nfunorge.org	Work: +47 22396050 Cell: +47 99624954 Fax: +47 22396063
Jenssen, Geir Brekke Mshauri wa Ufundi	Ministry of Health & Social Welfare Rehab unit, LNDC Block D Private Bag 222 Maseru 100 LESOTHO	jenssenseng@health.gov.ls geir@brekkejenssen.com	Work: +26622327009 Cell: +26685056105
Joelsdottir, Bergdis Mshauri wa Masuala ya Maendeleo	Norwegian Association of Disabled P.o Box 9217 Grønland 0134 Oslo NORWAY	bergdis.joelsdottir@nhf.no	Work: +47 24102482 Cell: +47 92447059 Fax: +47 24102499

Kalumuna, Zefania Mratibu wa Elimu Maalum	P.O. Box 9121 Dar es Salaam TANZANIA	zefakalu@yahoo.co.uk	Cell: +255744565878
Kangwa, Patrick Mwalimu	P.O. Box 450151 Mpika ZAMBIA	patrickkkangwa@yahoo.com	Cell: +26096802325
Khateli, Mathemoho Mkufunzi	Lesotho College of Education P.O. Box 0379 Maseru 105 LESOTHO	mpk93@yahoo.com	Work:+266 22312721 Home:+266 22325627 Cell: +266 22312721
Kotta, Jennifer	UNESCO P.O. Box 31473 Dar es Salaam TANZANIA	dar-es-salaam@unesco.org i.alima-kotta@unesco.org	Work: +255(22)2666623 /2667165 Fax: +255(22)2666927
Kulwa, Benjamin Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Elimu Maalum	Ministry of Education Special Needs Department P.O. Box 9121 Dar es Salaam TANZANIA	zefakalu@yahoo.co.uk	Cell: +255 744308502
Langlo, Ragna (Bikko) Kamati ya Utendaji ya Taifa	NORWAY	bikko@frisurf.no	Cell: +47 92098856
Lewis, Ingrid Afisa wa Utafiti na Maendeleo	Enabling Education Network (EENET) c/o Educational Support and Inclusion School of Education University of Manchester Oxford Road Manchester M139PL UK	ingridlewis@eenet.org.uk	Work:+44(0)1612753711 Cell: +44(0)7929326564 Fax: +44(0)1612753548
Mariga, Lilian Mshauri wa Mkoa, NFU	No. 2-51 st Avenue, Haig Park Mabelreign Harare ZIMBABWE	nfu@africaonline.co.zw	Cell: +2634306253

Massae, Evena Mratibu	TAMH P.O. Box 71434 Dar es Salaam TANZANIA	massae_evena@yahoo.com tamh.iep@bol.co.tz	Work: +255222775225 Cell: +255744578593
Matsie, Nthama Mwalimu-mahiri wa Wilaya ya Mafeteng	P.O. Box 550 Mafeteng 900 LESOTHO	i_matsie@yahoo.com	Work: +26622700213 Cell: +26658099354
Meisfjord, Ragnhild Mshauri	NORAD Education Unit P.O. Box 8034 Dep. 0030 Oslo NORWAY	ragnhild@meisfjord.com rame@norad.no	Work: +47 22240548
Menya, Charles O. Afisa-Projekti wa Elimu-Jumuishi, Oriang	Leonard Cheshire International East and North African Region P.O. Box 38748 00600 Nairobi KENYA	charlesmenya@yahoo.com	Cell: +254 722227981
Mulenga Mumba, Edwina Mwalimu	Kabale Basic School P.O. Box T144 Mpika ZAMBIA	chitimumba@yahoo.co.uk	Cell: +260 96827680
Muthaghawya, Beda Mwenyekiti	TAMH P.O. Box 71434 Dar es Salaam TANZANIA	tamh.iep@bol.co.tz	Work: +255 222775225 Fax: +255 222775225
Mwango, Noel Hillary Meneja-Kiongozi wa Elimu	Ministry of Education SNE Department Private Bag 328 Lilongwe MALAWI	noelmwango@yahoo.com	Work: +265 1788187 Cell: +265 8361610
Mwawesa, Samson Msimamizi wa Projekti, CBR	Salvation Army P.O. Box 535 Mbeya TANZANIA	mwaweza@yahoo.com	Cell: +255744527705

Mzee, Mussa Juma Mratibu	Zanzibar Association for People with Development Disabilities P.O. Box 4539 Zanzibar TANZANIA	zapdd@zanlink.com mussajuma36@hotmail.com	Work: +255242237527 Cell: +255777861724
Maalim, Mpaji Ali Afisa wa Elimu Maalum	Ministry of Education and Vocational Training Special Needs Education P.O. Box 394 Zanzibar TANZANIA	spned@zanlink.com	Cell: +255 777437569 Fax: +255 2234546
Namangale, Tommy J.D Meneja-Elimu wa Wilaya	Balaka District Education Office P.O. Box 354 Balaka MALAWI	Can be reached through Noel Mwango: noelmwango@yahoo.com or Victor Luwambala, MACOHA: vluwambala@macoha.org	Work: +265 545244 Cell: +265 8343130
Obeid, Fabian Hofi Mwenyekiti	ZAPDD P.O. Box 4539 or P.O. Box 1477 (private) Zanzibar TANZANIA	zapdd@zanlink.com obediminani@hotmail.com	Work:+255 242237527 Cell: +255 741428233 Fax: +255 242237527
Odwar, Henry Mwenyekiti wa Projekti ya Elimu- Jumuishi na Mkuu wa Shule, Oriang	P.O. Box 17 40223 Kadongo KENYA	Can be reached through: charlesmenya@yahoo.com or orpatieno@yahoo.com	Cell: +254 722584619
Pulumo, Mathabo Mkaguzi Msaidizi	Queen II Hospital P.O. Box 9494 Maseru 100 LESOTHO	mpulumo@webmail.co.za	Work: +27 58953377
Shindano, Othman Mkaguzi wa Elimu	Education Department Inspectorate Zanzibar TANZANIA		Cell: +255 777486630

Simango, Ellena Gertrude Meneja –Elimu wa Wilaya	District Education Office Blantyre Rural P.O. Box 11 Lunzu MALAWI	Can be reach through Noel Mwango: noelmwango@yahoo.com or Victor Luwambala, MACOHA: vluwambala@macoha.org	Work: +2651694411 Cell: +2659511495
Thorgersen, Line Mshauri wa Fedha	The Atlas-Alliance P.O. Box 9218 Grønland 0134 Oslo NORWAY	atlas@atlas-alliansen.no	Work: +47 23163593 Cell: +47 98476376
Tillya, Hugoline Mtaalam wa Majeraha, Mifupa na Misuli	Salvation Army P.O. Box 1273 Dar es Salaam TANZANIA	kikotillya@yahoo.com	Cell: +255744856651
Wadenya, Charles Afisa Elimu wa Wilaya	Busia District Local Government Department of Education P.O. Box 124 Busia UGANDA	wadenyacharles@yahoo.com	Work: +256712610699 Cell: +256772415043
Wadi, Uleid Juma Naibu Afisaelimu Kiongozi	Ministry of Education and Vocational Training P.O. Box 394 Zanzibar TANZANIA	spned@zanlink.com	Cell: +255773186107
Wormnæs, Siri Mtafiti	University of Oslo Department of Special Needs Education P.O. Box 1072 Blindern 0316 Oslo, NORWAY	siri.wormnæs@isp.uio.no	Work: +47 22858146

Mapendekezo ya marejeo

“Enabling Education” – the EENET newsletter. [Kuwezesha Elimu – makala ya EENET]. Namba 1-10 (EENET, 1997-2006)

Makala hizi zina makala fupifupi na rahisi kusoma. Zinahusu masuala ya elimu-jumuishi kwa mapana zaidi kutoka duniani kote. Zinaweza kusomwa kwenye tovuti: www.eenet.org.uk au zinapatikana kwenye CD-ROM kutoka EENET. Baadhi ya matoleo yake yanapatikana pia katika Breili na kanda za kusikiliza.

“Inclusive Education: Where there are few resources” [Elimu-jumuishi: Pale palipo na uhaba wa rasilimali] (Sue Stubbs / Atlas Alliance, 2002)

Kitabu hiki kinaonesha kwa ufasaha midahalo na vitendo/mazoezi kuhusu elimu-jumuishi – kwa kuzingatia zaidi nchi maskini.

“Learning from Difference: An action research guide for capturing the experience of developing inclusive education” [kujifunza kutokana na Makosa: Mwongozo wa utafiti wa kupata uzoefu wa kuanzisha elimu-jumuishi] (EENET, 2005)

Mwongozo huu unawawezesha wataalam na wanajamii kuaksi na kurekodi uzoefu/matendo yao, na kisha kujenga mawazo mapya na kufanya matendo/mazoezi mapya ili kuifanya elimu iwe jumuishi zaidi. Unatumia mazoezi-shirikishi sawa na yale yaliyotumiwa wakati wa warsha ya ‘Elimu-jumuishi kwa Vitendo’. Mwongozo huu unapatikana kwenye CD-ROM au printi (CD-ROM ina vifaa vingine vya zaida kama vile usuli katika kusoma, klipsi za video na za kusikiliza bila video, n.k.).

“Researching our Experience” [Kutafiti uzoefu wetu] (EENET, 2003)

Huu ni mkusanyiko wa makala fupifupi za walimu wa shule ya msingi Mpika, Zambia. Walimu hawa wamekuwa wakitumia utafiti kwa miaka mingi. Wanaelezea kuhusu changamoto walizokumbana nazo katika kuzifanya shule zao ziwe jumuishi zaidi, na ufumbuzi wa matatizo waliyokuwa wakipata wao pamoja na wafanyakazi wenzao, wanafunzi na wazazi.

“Schools for All: Including disabled children in education” [Shule kwa Wote: Pamoja na watoto walemavu katika elimu] (Save the Children, 2002)

Kitabu hiki cha mazoezi kinaonesha mawazo na baadhi ya masimulizi kutokana na uzoefu wa miaka mingi wa mashirika ya “Save the Children” na “EENET” katika elimu-jumuishi. Kuna pia kipeperushi kinchoonesha ufupisho wa mambo muhimu. Kitabu hiki kinapatikana kwenye mtandao, tovuti: www.eenet.org.uk au kwenye CD-ROM kutoka EENET. Nakala za Breili na kanda za kusikiliza zinapatikana pia. Kipeperushi kinapatikana EENET au NAD.

Kuhusu wafadhili na waandaaji wa warsha...

The Atlas Alliance

“The Atlas Alliance” ni shirika mwavuli na chombo cha kuratibu shughuli za kimataifa za maendeleo zinazofanywa na mashirika ya walemavu (DPO’s) nchini Norway. Muungano huo uliundwa mwaka 1981. Kwa sasa muungano huo una mashirika 14 na mawili ni mashiriki-shiriki. Mashirika ya NFU na NAD (angalia chini) ni wanachama wa DPO wa Muungano.

The Atlas Alliance
P.O. Box 9218, Grønland
0134 Oslo
Norway
Tel: +47 22174647
Fax: +47 23 16 35 95

E-mail: atlas@atlas-alliansen.no
Website: www.atlas-alliansen.no



NFU

Chama cha watu walemavu cha Norway (kifupi chake ‘NFU’ kwa ki-Norwei) ni shirika lisilo la kiserikali linaloshughulikia watu wasiojiweza. Wanachama wake ni pamoja na watu walemavu, ndugu zao na marafiki. Shabaha za ‘NFU’ ni jamii-jumuishi kwa wote. Tangu mwaka 1981 ‘NFU’ imekuwa ikishiriki katika maendeleo na mashirika-dada barani Afrika, Asia, Amerika ya kati na Karibiani. Lengo kuu limekuwa ni kuimarisha na kutetea haki za watu wenye ulemavu katika nyanja zao zote za maisha.

NFU
P.O. Box 8954 Youngstorget
N-0028 Oslo
Norway
Tel: +47 22 39 60 50
Fax: +47 22 39 60 60

E-mail: firmapost@nfunorge.org
Website: www.nfunorge.org



NAD

Chama cha Norway cha wasiojiweza (NAD) ni shirika linalofanya kazi kutetea haki sawa na kushirikishwa kikamilifu watu wasiojiweza nchini Norway. Kwa miaka 25 limekuwa likishirikiana na mashirika mengine ya maendeleo duniania dhidi ya mifumo yote ya ubaguzi na ukandamizaji

NAD
P.O. Box 9217, Grønland
N-0134 Oslo
Norway
Tel: +47 24 10 24 00
Fax: +47 24 10 24 99

E-mail: nhf@nhf.no
Website: www.nhf.no



Operation Day's Work

Kazi ya Siku ya Operesheni ni kampeni ya mshikamano ya kila mwaka inayofanywa na wanafunzi wa sekondari na elimu ya juu nchini Norway. Zaidi ya wanafunzi 115,000 hushiriki kwa kukaa siku moja bila kwenda shule, ili kupata kazi ya siku moja baada ya kampeni kamambe ya taifa. Mshahara wanaolipwa unachangia miradi ya elimu inayonufaisha au kusaidia vijana katika nchi zinazoendelea. Kila mwaka dola za ki-Mareakani milioni 3 mpaka 4 hukusanywa.



OPERASJON
DAGSVERK

Operation Day's Work

P.O. Box 8964, Youngstorget

0028 Oslo

Norway

Tel: +47 22 99 37 10

E-mail: od@od.no

Fax: +47 22 99 37 01

Website: www.od.no

EENET

Mtandao wa kuwezesha Elimu (The Enabling Education Network) ni mtandao unaoshirikiana habari kuhusu elimu-jumuishi; ni wazi kwa kila mtu. Wanachama wa mtandao huu ni walimu, wazazi, wanafunzi, mashirika ya siyo ya kiserikali, na wapanga-sera (serikalini). 'EENET' ina lenga zaidi elimu-jumuishi katika nchi za kusini (zinazoendelea), na kuendeleza na kuchangia habari na taarifa za kimaandishi zinazotolewa katika nchi hizi. Jarida la kila mwaka "Enabling Education" (kuwezesha Elimu) na tovuti yake kubwa ya www.eenet.org.uk ni vyombo mahsusi na vikuu vya mawasiliano vya mtandao huu wa "EENET".



EENET – The Enabling Education Network

c/o Educational Support and Inclusion

School of Education, University of Manchester

Oxford Road, Manchester M13 9PL

UK

Tel: +44 161 275 3711

Email: info@eenet.org.uk

Mobile: +44 7929 326 564

Website: www.eenet.org.uk

Fax: +44 161 275 3548



The Atlas Alliance
Schweigaardsgt 12
PO Box 9218 Grønland
0134 Oslo, Norway
Tel: +47 22 17 46 47
Fax: +47 23 16 35 95
Email: atlas@atlas-alliansen.no
www.atlas-alliansen.no

